



MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH MZIMA

SHEIKH ABDULAZIZ BIN ABDILLAH BIN BAAZ

USHEREHESHAJI WA MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH MZIMA

MTUNZI

SHEIKH ABDULAZIZ BIN ABDILLAH BIN BAAZ
(Allah amrehemu na amweke pahala pema peponi)

MSHEREHESHAJI

SHEIKH HAITHAM BIN MUHAMMAD JAMIL SARHAN
(Aliyekuwa mwalimu kwenye chuo cha Haram kwenye Msikiti wa Mtume Madinah na pia
msimamizi wa tovuti ya elimu ya Attasseel)
<http://attasseel-alelmi.com>
(Allah amsamehe na wazazi wake na waliohusika katika uandalizi wa kitabu hiki)

Chapa hii imetolewa kama waqf kwa ajili ya Allah
Kimechapishwa kwa udhamini wa Fatuma bint Jeilan bin Farihah (Allah amrehemu)

KIMEFASIRIWA KWA KISWAHILI NA
SULEIMAN MUHAMMED
Mwanafunzi Mkenya wa Chuo Kikuu cha Madinah, KSA.

CHAPA CHA KWANZA

Haki zote zimehifadhiwa

**Anayetaka kutoa chapa au kukifasiri kwa lugha nyingine kwa lengo la kukigawanya bure
baada ya kupata idhini kutoka kwa mtunzi basi awasiliane na
islamtorrent@gmail.com**

Kitengo cha Ujumbe

Sharh ya Utangulizi wa Mtunzi

Amesema Sheikh Abdulaziz bin Abdillahi bin Baaz, Allah amrehemu:

Bismillahi Rahmani Rahim

Shukrani zote ni zake Allah Mola wa walimwengu, na mwisho mwema ni kwa wacha Mungu. Kisha rehema na amani zimwendee Mja wake na Mtume Wake nabii wetu Muhammad, na waliomfuata na Sahaba zake kwa jumla.

Baada ya hayo:

Hakika haya ni maneno yaliyofupishwa katika kubainisha baadhi ya mambo yanayolazimu ummah wote kuyatambua katika Uislamu, nimekiita:

MAFUNZO MUHIMU KWA UMMAH WOTE

Namuomba Allah anufaishe nacho Waislamu na aitakabali kutoka kwangu, hakika yeye ni Mkwasi Mkarimu.

Abdulaziz bin Abdillahi bin Baaz

Mbona tunakisoma kitabu cha Mafunzo Muhimu?

Tunakisoma kwa sababu ni muhimu kama alivyokiita Mtunzi na Maulamaa wengi wakakihusia kusomwa.

Na yeyote akiuliza: Hiki ni kitabu cha ummah mzima, na mimi ni mwanafunzi wa elimu ya dini, cheo changu kiko juu kuliko waliobaki katika jumla ya ummah.

Jibu: Tutamuuliza kilichoko ndani ya kitabu hiki. Akishindwa kulijibu basi jumla ya ummah waliobaki ni bora kumliko yeye. Na yampasa mwanafunzi wa elimu awe mnyenyekevu na wala asiwe ni mwenye kiburi kwenye elimu na maulamaa. Na afuate mkondo wa maulamaa waliobobea.

Na katika (Sahih Bukhari): Amesema Mujahid: ***Hatopata elimu mwenye haya na mwenye kiburi.***

Ni yapi yaliyomo katika kitabu cha Mafunzo Muhimu?

- Njia za wema waliotangulia katika kuisoma Kur’ani, kuihifadhi, kuizingatia na kuitendea kazi
- Kubainisha Uislamu, Imani, Ihsani, Tauhidi na aina za Shiriki
- Kubainisha Sala
- Kubainisha Wudhuu
- Kusifika kwa nidhamu za kidini na kuwa na tabia na adabu njema za Kiislamu
- Kutahadhari na Ushirikina na aina za Maasi
- Maandalizi ya maiti, kumswalia na kumzika.

Mbona maulamaa wengi huanza uandishi wao kwa: Bismillahi Rahmani Rahim?

Kuiga mfumo wa
Kur’ani Tukufu,
Manabii na
Mitume, rehema
na amani ziwe juu
yao

Kuitekeleza
hadith inayosema:
**“Kila jambo
lenye zao ambalo
halitaanza kwa
jina la Allah basi
limeporomoka”**

Japo hadith
yenyewe ni
dhaifu.

Kuiga Maulamaa
wema
waliotangulia,
Allah awarehemu.

Kwa matarajio
ya kupata mema
na baraka kwa
kuanza kwa jina
la Allah
aliyetukuka.

SOMO LA KWANZA

SURATUL FATIHAH NA SURAH ZINGINE FUPI

Suratul Fatihah na surah zingine fupi, kuanzia Suratul Zalzala mpaka Suratu Naas kwa udhibiti, kurekebisha usomaji, kuhifadhi na kusherehesha yanayopaswa kufahamika.


UFAFANUZI

Maanake aihifadhi – kama walivyokuwa wema waliotangulia – kila siku aya kumi pamoja na kusoma tafsiri zake kuanzia tafsiri za mukhtasar kwa mfano Tafsiri ya Abdurahman Saadiy, Allah amrehemu na amsamehe madhambi yake. Ajifunze nacho na akitendee kazi.

MWANAFUNZI ANAFAA KUANZA KWA TAFSIRI IPI?

Mwanafunzi wa elimu ya dini anahusiwa aanze kwa ((Taisiril Karimi Rahman fii Tafsiri kalaamil Mannan)) cha Sheikh Abdurahman bin Nassir As-Saadiy, Allah amrehemu.

MBONA MWANAFUNZI ANAFAA KUANZA NACHO?



AINA ZA WATU KATIKA KUAMILIANA NA KUR'ANI

Watu wamegawanyika katika kuamiliana na Kur'ani makundi matatu

WAADILIFU

Hiki ni kikundi kinachodumu katika kuisoma Kur'ani, kuhifadhi, kuzingatia na wanamuomba Allah kuwawezesha kuitekeleza kwa vitendo.

Na hii ndio ilikuwa hali ya wema waliotangulia

WASIOZINGATIA

Hawa ni wale wanaosoma na kuhifadhi bila mazingatio wala vitendo

WALIOIHAMA

Hiki ni kikundi kilichoihama Kur'ani.

Na kuihama Kur'ani inakuwa kwa mambo yafuatayo:

Kutoisoma

Kutohifadhi

Kutozingatia

Kutofanyia kazi

Kutojitibu nayo kwa maradhi ya

Anasema Allah, **“Na atasema mtume (siku ya kiyama): ewe Mola wangu, hakika ya kaumu yangu waliihama hii Kur'ani.”** na amesema Mtume, rehma na amani ziwe juu yake, akiashiria kiongozi wa kikundi cha watu walioenda kinyume na mafunzo yake, *“hakika katika kizazi chake watatoka watu wanaosoma Kur'ani na wala haivuki kinywa chao. Watawaua Waislamu na kuwaacha wale wanao abudu masanamu. Na hakika watatoka katika Uislamu kama vile mshale utoka kwenye upinde. Lau ningefikia zama zao ningewapiga vita vikali.”*

Chemichemi kutoka kwa kitabu cha Tafsiri cha Sheikh Abdurahman bin Nassir As-Saadiy, Allah amrehemu na masuali juuya hayo.

[TAFSIRI YA SURATUL FATIHAH]

(Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah)

(1). Bismillahi Rahmani Rahim. (2). Alhamdu Lillahi Rabbil Alamin. (3). Arrahmani Rahim. (4) Maliki yaumid diin. (5). Iyyaka na 'budu wa iyyaka nasta 'iin. (6). Ihdinaa swiratwal mustaqim. (7). Swiratwa ladhina an amta aleihim, ghairil magh-dhubi aleihim wa la dhwaallin.

(Aya 1): Surah hii imeanza kwa kila jina lake Allah. Kwa sababu Allah ni neno linalokusanya majina yote mazuri yake Allah. Jina **Allah** linamaanisha anayestahiki kupwekeshwa kwenye ibada, kutokana na sifa za ukamilifu anazozimiliki katika uungu Wake. **(Ar-Rahmani Ar-Rahim)** haya ni majina mawili Yake Allah ambayo yanaonyesha kuwa Allah ametakasika na anasifika kwa upana wa rehema inayopenya kwa kila kiumbe kilichoko hai. Na akaiwekea fungu bora maalum aliyowaandikia waja Wake waumini walioiga mienendo ya Manabii an Mitume; hawa watapata fungu maalum ya rehema ambayo imeandaliwa rasmi kwa ajili yao.

Na utambue kwamba miongoni mwa misingi waliokubaliana wema waliotanguliwa na wanazuoni wote ni; kuiamini majina yake Allah na sifa Zake na kanuni za sifa hizo. Kwa mfano: wanaamini kuwa Allah ni mwenye rehema, mwenye kurehemu; anasifika kwa rehema kwa kila kiumbe, basi kutokana na hayo athari na matokeo ya rehema Zake tunapata neema. Na vile vile kwa majina Yake yaliyobaki.

Husemwa katika jina Lake, **Mjuzi wa yote:** Allah ni mwenye elimu wa kila kitu. **Mweza:** mwenye uwezo juu ya kila jambo.

(Aya 2): *Alhamdu Lillahi* **(Shukrani zote ni Zake Allah):** Ametukuka na ametakasika Allah kwa kila sifa ya ukamilifu, na kwa matendo Yake ambayo yako baina ya fadhila na uadilifu; ametakasika Allah kwa kila namna.

Rabbil Alamin (Mola wa walimwengu): Rabb inamaanisha Mola. Rabb kwa asili ya lugha ya Kiarabu inamaanisha mlezi. Kwa hiyo Allah ni Mlezi wa vyumbe vyote; kwa kuviumba, kuviandaa, kuvineemesha kwa neema kubwa ambazo lau zingekosekana, ingepelekea kukosekana maisha. Kila neema inatoka kwa Allah. Na malezi ya Allah kwa vyumbe vyake yamegawanyika aina mbili:-

1. **Malezi ya Jumla:** Haya ni malezi ambayo Allah amewapa vyumbe wote; kwa kuwaumba, kuwaruzuku na kuwaongoza kwa kila lenye maslahi kwao katika maisha yao ya Duniani.
2. **Malezi Maalum:** Haya ni malezi maalum kwa wanaomcha Allah: Allah anawalea malezi maalum katika Imani, kuwajaalia ufaulu, kuwapa ukamilifu wa Imani na kuwaepusha na misukosuko, dosari na vizuizi baina Yake na wao. **Uhalisia wa Malezi Maalum:** Kuwawezesha katika kila kheri na kuwaepusha na kila shari. Na huenda hii ndio siri katika dua za Manabii kutumia kwao neno Rabb; kwa sababu haja zao zote zilikuwa katika malezi maalum. Basi **Rabbil Alamin** inaonyesha kumpwekesha Allah katika *uumbaji, uendeshaji, neema, ukwasi wake Allah na ufakiri wa vyumbe kwa kila njia*.

(Aya 4): Maliki yaumid diin (Mfalme wa Siku ya Malipo): Malik inamaana ya mfalme. Hii inaonyesha kuwa Allah anasifika kwa ufalme bila mipaka; ufalme ambao ana uwezo wa kuamrisha, kukataza, kulipa na kuadhibu bila mipaka. Anatawala katika ufalme Wake kwa uhuru mkamilifu wa utawala. Kisha Allah akaegemeza ufalme kwa siku ya malipo (Kiyama) ambayo ni siku watakayolipwa wanadamu kwa kila walilotenda ya mema na uovu. Ni siku ambayo itadhihirika kwa vyumbe wote ukamilifu wa ufalme Wake Allah, uadilifu Wake, Hukumu Zake na mwisho wa umiliki wa vyumbe. Siku hiyo watakuwa hali sawa wafalme na raia, watumwa na waliokuwa huru; wote watanyenyekea utukufu Wake Allah wakisubiri malipo ya yale waliyoyatenda, wakitajarajia thawabu Zake Allah, wakihofia adhabu Yake. Ndiposa Allah akaegemeza ufalme Wake kwa kutaja siku ya malipo.

(Aya 5): *Iyyaka na 'budu wa iyyaka nasta 'iin* (Ni Wewe tu tunakuabudu na ni Wewe tu tunakutaka msaada): Maanake: Tunakupwekesha ewe Allah kwa ibada na kutaka msaada. Kwa sababu katika ufundi wa lugha ya Kiarabu, neon **Iyyaka** inapotangulizwa mbele ya kitendo inakuwa na maana ya kupwekesha kitu kwa hicho kitendo.

Ibada ni neno linalokusanya kila jambo ambalo Allah analipenda na analiridhia kutokana na vitendo na kauli zilizo wazi na zilizofichika.

Kumtaka Allah msaada ni kumtegemea Allah katika kuleta manufaa na kuzuia madhara pamoja na kuwa na imani ya kufikia hayo malengo.

Kutekeleza ibada na kumtaka Allah msaada ndio njia ya kuweza kupata furaha na kuongoka kutokana na aina zote za shari; hakuna njia ya kuongoka isipokuwa kwa kutekeleza ibada na kumtaka Allah msaada. Na ibada inakuwa yenye mazingatio ikifanywa kutokana na mafunzo ya Mtume, rehema na mani ziwe juu yake, na ikikusudiwa radhi Zake Allah pekee. Kwa kuzingatia haya mawili, ibada inakuwa ibada sahihi. Kisha Mtunzi akataja kumtaka Allah msaada baada ya kutaja ibada, pamoja na kuwa inaingia kwenye ibada, kwa sababu mja anahitaji msaada wa Allah katika kila ibada; na akiukosa msaada wa Allah hatoweza kufikia matakwa yake katika kutekeleza maamrisho na kuepuka makatazo.

(Aya 6): *Ihdinsa Swiratwal mustaqiim* (Tuongoze kwenye njia iliyonyooka): Maana ya aya: tuonyeshe, tueongoze na utuwezeshe kwenye njia iliyonyooka; njia iliyonyooka ni njia iliyo wazi na yenye kumpeleka mja kwa Allah na pepo Yake, na hii inakuwa kwa kuijua haki na kuitendea kazi. Tuongoze kwenye njia na tuongoze ndani ya njia. Kuongozwa kwenye njia ni ni kushikamana na dini ya Uislamu na kuikufuru dini zingine zote. Na kuongozwa ndani ya njia ni kuongoka katika mambo yote ya kidini, kielimu na vitendo. Na hii aya ni dua iliyokusanya vyote vya muhimu na yenye manufaa zaidi. Ndio maana imewajibika juu ya kila mwanadamu kumuomba Allah katika kila rakaa ya swala yake kwa udharura wake. Na hii njia ni

(Aya 7): *Swiratwa ladhina an amta aleihim* (Njia ya wale uliowaneemesha): njia ya walioneemeshwa katika manabii, wakweli, mashahidi na wema.

Ghairil (sio njia ya wale) magh-dhubi aleihim (uliowakasirikia): wale waliojua haki na wakaiwacha kama Mayahudi na mfano wao. Na wala sio njia ya **Adh-dhwalliin (waliopotea):** wale waliowacha haki kwa ujahili na upotovu kama Wakristo na mfano wao.

Hakika ya hii surah, pamoja na ufupisho wake, imekusanya mambo ambayo surah nyingine za Kur’ani hazijakusanya. Ndani yake mnapatikana aina tatu za Tauhidi: 1. Kumpwekesha Allah katika Malezi Yake kama ilivyoko kwenye kauli Yake **Rabbil alamin**. 2. Kumpwekesha Allah katika uungu Wake – ibada Yake –kama ilivyo kwenye kauli **Yake Iyyaka na’budu wa iyyaka nasta’iin**. 3. Kumpwekesha Allah katika majina Yake na sifa Zake; kumthibitishia sifa za ukamilifu ambayo amejithibitishia na amemthibitishia bila ya kuzigeuza, kuzipinga, kuzishabihisha wala kuzitolea namna. Na hii tumeipata kwenye kauli Yake **Alhamdu**.

Pia surah hii imebeba ndani yake uthibitisho wa utume katika kauli Yake **Ihdinas Swiratwal mustaqiim**. Maana hili haliwezi timia bila Mtume wa kuelekeza kwenye njia hii ilinyooka.

Pia ndani yake kuna uthibitisho wa malipo ya matendo kama ilivyo kwenye kauli Yake **Maliki yaumid diin**, na hakika ya malipo yatakuwa kwa uadilifu.

Pia imepatikana ndani yake uthibitisho wa Qadar na kwamba mja ni mtendaji.

Pia imewaponda watu wote waliozama katika uzushi na upotovu kwa kauli Yake **Ihdinas Swiratwal mustaqiim**; kwa sababu ndio njia kuijua haki na kuitendea kazi na yeyote mzushi na mpotovu yupo kinyume na haya.

Pia imepatikana ndani yake maamrisho ya kuipwekesha dini kwa Allah katika kumuabudu Yeye pekee na kumtaka Yeye pekee msaada kama ilivyo kwenye kauli Yake **Iyyaka na’budu wa iyyaka nasta’iin**.

Shukrani zote zimrudie Allah, Mola wa walimwengu.

[TAFSIRI YA AYATUL KURSI]

Allahu laa ilaha illa huwal Hayyul Qayyum, laa ta'khudhuhu sinatu wa laa naum. Lahu maa fis samawati wa maa fil ardh. Man dha ladhii yashfa^u ^indahu illa bi idhnihi. Ya^lamu ma baina aidihiim wa maa khalfahum. Wa laa yuhitwuuna bishein min ^ilmihi illa bimaa shaa. Wasia^ kursiyyuhus samawati wal ardh. Wa laa yauduhu hifdhuhumaa wa huwal ^Aliyyul ^Athwiim (Baqarah 255).

Ameelezea Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuwa hii aya ndiyo aya kubwa katika Kur'ani; kutokana na maana za Tauhidi, ukubwa wa Allah na sifa za ukamilifu zinazopatikana ndani yake. Ameelezea Allah kuwa: *Allah* ambaye anastahiki maana zote za Uungu, na kuwa hakuna apasaye haki ya kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye Allah pekee Yake; basi kuabudu miungu mingine hiyo ni ibada potovu. Na ya kuwa Yeye Allah ni *Al-Hayyu* ambaye anamiliki sifa zote za maisha kamilifu kama kusikia, kuona, uwezo, kutaka na sifa zingine zinazohusiana na Dhati Yake, kama vile Yeye ni *Al-Qayyum* sifa ambayo inabeba sifa zote za vitendo; kwa sababu *Al-Hayyu* ni Yule anayejitegemea mwenyewe wala hana haja kumtegemea kiumbe yeyote. Ameumba viumbe waote vyote na akavipa kila wanavyohitaji katika maisha. Allah ni qayyum ambaye amtakasika katika vitendo vyake na ameepukana na sifa za upungufu, ndio maana akasema *laa ta'khudhuhu sinatu* (hasinzii) *wa laa naum* (haimchukui usingizi). Sifa ya kusinzia na kulala ni sifa mbili zinazompata kiumbe ambaye hupatwa na udhaifu, unyonge na uchovu na wala hazimpatii mwenye sifa ya Utukufu, Ukubwa na Uwezo.

Kisha Allah akaelezea kuwa anamiliki yote yaliyomo mbinguni na ardhini, kila kitu ni mtumwa wa Allah na milki yake wala hakuna hata kimoja kinachoepuka kutoka kwa ufalme Wake kama anavyosema katika Kur'ani (*Kila aliye mbinguni na ardhini atamjia Allah siku ya Kiyama akiwa mja*). Allah ndiye mmiliki wa vyote vilivyomo. Yeye Allah pekee ndiye mwenye sifa ya ufalme, uendeshaji, uwezo na utukufu. Na katika ukamilifu wa ufalme Wake hakuna yeyote *yashfa^u ^indahu* (**anayeweza kumtakia yeyote maombezi**) *illa biidhnihi* (**isipokuwa kwa idhini Yake**). Kila muombezi ni mwelekezi ni mja wa Allah na yupo katika ufalme Wake na wala hatokubaliwa kukadimisha maombezi yake ila kwa idhini Yake. Anasema Allah katika Kur'ani (*Hakika maombezi vote ni*

.
Nayo ni Yake ufalme wa mbingu na ardhi). Na Allah hatompa yeyote idhini ya maombezi isipokuwa yule aliyemridhia, na hatomridhia yeyote isipokuwa mwenye kumpwekesha katika Tauhidi na akawafuata Mitume Wake Allah. Basi asiyekuwa na hizi sifa hatopata fursa ya maombezi siku ya Kiyama.

Kisha Allah akaendelea kuelezea kuwa elimu Yake ni pana yenye kukusanya kila kitu na kuwa Yeye ni mjuzi wa yale yote yanayowahusu viumbe katika mambo ya mustakbali wao na yale *wa maa khalfahum* (**yaliyopita**) katika mambo yaliyopita yasiokuwa na mipaka; na wala hakuna lolote linalomponyoka (*Allah ni mjuzi wa yote yanayodhihirika machoni na yaliyofichika vifuani*) na wala hakuna kiumbe chochote kinachoweza kuitambua elimu na ujuzi wa Allah hata lepe *illa bima shaa* (**alichowajaalia Allah**) katika hayo; nayo ni yale aliyowavumbulia katika mambo ya sharia na Qadar (nacho ni kipande kidogo sana ukilinganisha na elimu ya Allah kama walivyomsifu malaika na Mitume (*Umetukuka. Hatuna elimu isipokuwa yale uliyotuelimisha*))

Kisha Allah akaelezea utukufu Wake na kuwa kursi Yake imepiku kwa ukubwa mbingu na ardhi, pamoja na kuwa amezihifadhi mbingu na ardhi na wote waliyomo ndani ya mbingu na ardhi amewahifadhi kwa njia na nidhamu ambazo amewajaalia. Lakini pamoja na hayo, haimshindi kuhifadhi mbingu na ardhi kwa sababu ya ukubwa Wake, utukufu Wake, uwezo Wake na upana wa hekima katika hukumu Zake, naye ni *Al-Aliyyu* (**Yupo juu**) katika dhati Yake na katika ukubwa Wake na Yupo juu ya viumbe wote na kila kilichopo kinamnyenyekea na kinajidhalilisha kwa *Al-Athwiim* (**Mtukufu**) aliyejumuisha sifa zote za kutakasika na kutukuka, ambaye nyoyo zinampenda, zinamtakasa nafsi na wanatambua wajuzi kuwa kila kitu pamoja na ukubwa wake ila kinanyenyekea kwake Allah.

Aya hii imekusanya maana kubwa ambayo inaifanya aya kubwa katika Kur'ani na ni haki ya kila mwenye kuisoma kwa mazingatio na ufahamu aijaze moyo wake kwa yakini, ujuzi na imani, na anakuwa amehifadhika kutokana na shari za shetani.

[TAFSIRI YA SURATU IDHAA ZULZILAT]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

- (1). *Idhaa zulzilatil ardhu zilzaalahaa.* (2). *Wa akhrajatil ardhu athqaalahaa.*
(3). *Wa qaalal insanu maa lahaa.* (4). *Yaumaidhin tuhaddithu akhbaarahaa.*
(5). *Bianna rabbaka auhaa lahaa.* (6). *Yaumaidhin yasdurun naasu ashtaatan*
liyurau a[^]maalahum. (7). *Famai ya[^]mal mithqaala dharratin khairai yarah.*
(8). *Wa mai ya[^]mal mithqaala dharratin sharrai yarah.*

(Aya 1-2): Anaelezea Allah kuhusu yale yatakayotokea Siku ya Kiyama na kuwa ardhi itatikiswa na kutetemeshwa kwa ushindo mkubwa utakaopelekea kuanguka kila jengo kilichopo ndani ya ardhi, na milima itaporomoka na kusawazishwa pasiwe na mnyanyuko wowote, *Wa akhrajatil ardhu athqaalahaa* (Na itakapotoa ardhi mizigo yake) katika maiti na madini.

(Aya 3): *Wa qaalal insaanu* (atasema mwanadamu) kwa anayoyaona katika hali ngumu ya dunia siku hiyo, *maa lahaa* (ina nini) leo dunia?

(aya 4-5): *Yaumaidhin tuhaddithu* (siku hiyo itaelezea) ardhi *akhbaarahaa* (habari zake) kwa iliyoshuhudia katika matendo ya wanadamu ya kheri na ya shari. Hakika ardhi itakuwa katika jumla ya mashahidi siku ya Kiyama. *Bianna rabbaka auhaa lahaa* (kwa sababu Mola wako ameamrisha) ameamrisha kuelezea vitendo vya waja.

(aya 6): *Yaumaidhin yasduru nnaasu* (siku hiyo watu watatoka) wametengana *liyurau a[^]maalahum* (matendo yao) waliyoyatenda ya mema na maovu.

(aya 7-8): *Famai ya[^]mal mithqaala dharratin khairan yarah. Wa mai ya[^]mal mithqaala dharratin sharran yarah* (atakayetenda mema kadri ya punje basi atalipwa. Na atakayetenda uovu kadri ya punje basi atalipwa) katika ya kheri na shari kwa sababu kila atakalofanya, kubwa na ndogo atalionga na atalipwa.

[TAFSIRI YA SURATUL AADIYAAT]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). *Wal aadiyaati dhawab-haa.* (2). *Falmuuriyaati qad-haa.* (3). *Falmughiiraati sub-haa.* (4). *Fa-atharna bihi naq'aa.* (5). *Fawasatna bihi jam-aa.*
(6). *Innal insaana lirabbihi lakanuud.* (7). *Wa innahu alaa dhaalika lashahiid.*
(8). *Wa innahu lihubbil khairi lashadiid.* (9). *afalaa ya'lamu idhaa bu'thira maa fil qubuur.* (10). *inna rabbahum bihim yaumaidhin lakhabiir.*

(Aya 1): Ameapa Allah, aliyetukuka, kwa farasi; kwa yanayopatikana kwake ya dalili kubwa na neema zilizo wazi wakati wanapokabiliana na maadui; dalili na neema hizi zinaptika tu kwa farasi. Amesema, *wal aadiyaati dhawab-ha* (naapa kwa farasi wendao mbio wakipumua) farasi wanaowakabili maadui kwa kishindo.

(Aya 2): *Falmuuriyaati qad-haa* (wakitoa moto kwa kupiga kwato zao chini): kwa kwato zao wakikanyaga mawe wakitoa moto kwa kushambulia.

(Aya 3): *Falmughiiraati* (wakishambulia) adui *sub-haa* (asubuhi) na hili ni jambo la kawaida kuwa mashambulizi yanakuwa asubuhi.

(Aya 4-5): *Fa-atharna bihi* (huku wakitimua) kwa kuwashambulia maadui zao *naq-aa* (vumbi) na kuingia katikati ya majeshi ya maadui.

(Aya 6): Alichokiapia Allah ni *innal insaana lirabbihi lakanuud* (hakika mwanadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola wake Mlezi) mbanifu wa kheri. Katika maumbile yake mwanadamu nafsi yake hairuhusu kutekeleza haki na amana iliyo juu yake. Na hupata uzembe katika kutekeleza hayo isipokuwa yule ambaye Allah amemuongoza na kumuepusha na sifa hii ndiye atatekeleza haki.

(Aya 7): *Wa innahu alaa dhaalika lashahiid* (na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo) hakika ya mwanadamu ni shahidi juu ya tabia ya nafsi yake ya kutotekeleza haki na amana, wala hawezi likanusha. Kuna onyo kali kwa mwenye tabia hiyo.

(Aya 8): *Wa innahu* (na hakika yeye) mwanadamu *lihubbil khairi* (katika kupenda mali) yaani mali *lashadiid* (ana nguvu); ni mwingi sana wa kupenda mali. Na kupenda kwake mali zaidi ndio kumempelekea kutotekeleza haki na amana; ametanguliza matamano yake juu ya majukumu yake ya kumridhisha Mola wake.

(Aya 9-10): Ndio maana Allah akasema kumuogopesha siku ya Kiyama *afalaa ya'lamu* (kwani hajui) huyu aliyeghurika *idhaa bu'thira ma fil qubuur* (watakapofufuliwa walioko makaburini) Allah atakapowatoa wafu makaburini kwa ufufuo *wa husswila maa fi ssuduur* (na yakakusanywa yaliyomo vifuani) yale yaliyokuwa yamesitiriwa nyoyoni katika mema na maovu yakawa dhahiri mbele ya viumbe wote.

(Aya 11): *inna rabbahum bihim yaumaidhin lakhabiir* (kwa hakika Mola wako Mlezi atakuwa na habari zao siku hiyo) anayajua yaliyofichika na yaliyo wazi katika matendo ya mwanadamu na atawalipa kwa hayo siku ya Kiyama.

[TAFSIRI YA SURATUL QAARIAH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). *Alqaariah*. (2). *Malqaariah*. (3). *Wa maa adraaka malqaariah*
(4). *Yauma yakuunu nnaasu kalfaraashil mabthuuth*. (5). *Wa takuunul jibaalu kal-ihnil*
manfuush. (6). *Fa ammaa man thaqulat mawaaziinuh*.
(7). *Fahuwa fii iishatin raadhwiyyah*. (8). *wa ammaa man khaffat mawaaziinuh*
(9). *Faummuhu haawiyah*. (10). *Wa ma adraaka maa hiyah*. (11). *Naarun haamiyyah*

(Aya 1-3): *Alqaariah* (inayogonga) hii ni moja katika majina ya siku ya Kiyama. Imeitwa hivi kwa sababu inashtua kwa kugonga kwa matukio yake.

(Aya 4): *Yauma yakuunu nnaasu* (siku ambayo watu watakuwa) kwa sababu ya uzito wa siku hiyo *kalfaraashil mabthuuth* (kama nondo waliotawanyika) wakatapakaa hewani.

(Aya 5): Ama milima siku hiyo itakuwa *kal-ihnil manfuush* (kama sufi zilizochambuliwa) kwa udhaifu wake na kuelea hewani siku hiyo kwa amri ya Allah.

(Aya 6-7): *Fa ammaa man thaqulat mawaazinuh* (basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito) kwa kuwa mema yake yakazidi maovu *fahuwa fii iishatin raadhwiya* (huyo atakuwa katika maisha ya kupendeza) ndani ya jannah.

(Aya 8-11): *Wa ammaa man khaffat mawaazinuh* (na yule ambaye mizani yake itakuwa hafifu) kwa kuzidi maovu yake kushinda mema *faummuhu haawiya* (huyo maskani yake yatakuwa moto wa Haawiya) makaazi yake. Haawiya ni katika majina ya jahanamu. Atatupwa ndani ya moto huo kwa uso wake ambao ni moto *haamiya* (mkali)

[TAFSIRI YA SURATU TTAKAATHUR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Alhaakumu ttakaathur (2). Hatta zurtumul maqaabir

(3). Kallaa saufa ta'lamuun (4). Thumma kallaa saufa ta'lamuun.

(5). Kallaa lau ta'lamuun ilmal yaqiin. (6). Latarawunnal jahiim.

(7).Thumma latarawunnahaa ainal yaqiin. (8). Thumma latus-alunna yaumaidhin ani nnaiim.

(Aya 1): Anasema Allah huku akimkemea mwanadamu kwa kushughulika na mambo mengi na kuliacha jukumu lake la kumuabudu Allah; ambalo ni lengo la kuumbwa kwake *alhaakumu ttakaathur* (**kumekushughulisheni kutafuta wingi**); kuzidisha mali, watoto, marafiki, vyeo na mambo mengine yasiyo ya msingi.

(Aya 2): Kughafilika na kushughulika huku kumeendelea *hatta zurtumul maqaabir* (**mpaka mje makaburini/mfe**) basi hapo ndipo anagutuka na kukumbuka lengo lake. Allah ametumia neno ziara katika maisha ya barzakh (kaburini) kwa sababu ni kivukio kwenda maisha ya akhera kwa hesabu na malipo.

(Aya 3-6): Ndio maana akawapa ahadi kali *kallaa saufa ta'lamuun.....* (**Sivyo hivyo. Mtakujajua.....**) lau mwanadamu angelijua lililo mbele yake katika akhera basi angeliacha linalomshughulisha na kurudi kwenye ibada na matendo mema kwa wingi.

(Aya 7): *Thumma latarawunnahaa ainal yaqiin* (**tena bila shaka mtakuja liona kwa jicho la yakini**) kwa jicho la hakika

(Aya 8): *Thumma latus-alunna yaumaidhin ani nnaiim* (**tena bila shaka mtakuja ulizwa siku hiyo juu ya neema**) mlioneemeshwa nayo duniani. Je mlishukuru na mkatekeleza haki ya Allah pasina kuzitumia katika maasi? Au mlizikufuru na mkazitumia katika kumuasi Allah na wala hamkutekeleza haki za Allah katika neema hizo?

[TAFSIRI YA SURATUL ASR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

*(1). Wal-asr. (2). Innal insaana lafii khusr. (3). Illa ladhiina aamanuu wa amiluu
sswaalihaati wa tawaaswau bilhaqqi wa tawaaswau bisswabr*

(Aya 1-3): Allah ameapa kwa asr (zama/muda) ambao ni usiku na mchana. Muda huu ndio pahala pa matendo ya mwanadamu. Allah amesema kuwa kila mwanadamu yupo kwenye aina zote za hasara isipokuwa mwenye sifa nne:-.

- **IMANI:** Anayemuamini Allah kwa yote aliyoamrisha kuaminiwa. Na imani haiwi bila ya elimu kwa sababu haitimii bila hiyo.
- **MEMA:** Anayetenda mema yaliyofichika na yaliyodhihirka katika kutekeleza haki za Allah na haki za waja za lazima.
- **KUHUSIANA HAKI:** Wakahusiana wenyewe kwa wenyewe katika jambo la haki ambalo ni imani na matendo mema.
- **KUHUSIANA SUBIRA:** Wakahusiana kufanya subira katika uchamungu, kutokana na maasi na katika mipango (Qadar) ya Allah.

Kwa kutekeleza mambo mawili ya mwanzo, mwanadamu atakuwa ameikamilisha nafsi yake na kwa kutenda mawili ya mwisho atakuwa amewakamilisha wenzake kuepuka hasara.

[TAFSIRI YA SURATUL HUMAZAH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). *Wailun likulli humazatin lumazah.* (2). *Alladhii jama-a maalahu wa a-ddadah.* (3). *Yahsabu anna maalahu akhaladah.* (4). *Kallaa layumbadhanna fil hutwamah.* (5). *Wa maa adraaka mal hutwamah.* (6). *Naarullaahil muuqadah.* (7). *Allatii tattwaliu alal af-idah.* (8). *Innahaa aleihim mu'swadah.* (9). *Fii amadin mumaddadah.*

(Aya 1): *Wailun likulli humazatin lumazah* (Ole wake kila safihi msengenyaji) hili ni onyo kali kwa wale wanaowaudhi na kuwaaibisha watu kwa vitendo na maneno. **Humaza** ni yule anayewaudhi watu kwa vitendo na **lumaza** ni anayeudhi kwa maneno.

(Aya 2): Na katika sifa za watu hawa, hawana linalowashughulisha zaidi ya kuchuma na kujumuisha mali huku wakipata furaha wanapozihesabu na wala hawazitumii katika yanayomfurahisha Allah.

(Aya 3): *Yahsabu* (anadhani) mwanadamu *anna maalahu akhladah* (kuwa mali yake yatambakisha milele) duniani. Ndio maana ikawa hamu yake kubwa ni mali na ubakhili na kuasahau kuwa haitomfaa katika maisha ya akhera na kwa hilo akawa ameharibu akhera yake na mema yake.

(Aya 4-7): *Kallaa layumbadhanna* (hakika huyo atavurumishwa) kwa uso wake ndani ya *Hutwama* (moto wa Hutwama) ambao kwa ukali wake *tattwaliu alal af-idah* (ambao unapanda moyoni) inachoma mwili hadi ndani ya nyoyo.

(Aya 8): Pamoja na ukali wa joto la moto huu na hali ngumu ndani yake, watakuwa *innahaa aleihim mu'swadah fii amadin mumaddadah* (hakiwa ndani ya moto huo watafungiwa kwenye nguzo zilizonyooshwa) nyuma ya nguzo za milango yake wasiweze kutoka kwa hali yoyote ile.

[TAFSIRI YA SURATUL FIIL]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Alam tara kaifa fa-ala rabbuka bi-as-haabil fiil . (2). Alam yaj-al kaidahum fii tadhwiil. (3). Wa-arsala aleihim twairan abaabiil. (4). Tarmiihim bihijaaratim min sijjiil. (5). Faja-alahum ka-asfim ma'kuul.

(Aya 1-5): Je! Hukuona, katika mipango ya Allah na uwezo Wake mkubwa na dalili za kupwekeshwa Kwake na kusadikisha utume wa Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, alivyowafanya watu wa ndovu; ambao walikaribia Nyumba Yake tukufu na wakataka kuibomoa. Wakaandaa jeshi kubwa wakiwa na ndovu wakubwa kwenye jeshi lao kwa lengo la kuibomoa Kaabah. Wakaja kwa jeshi kubwa kutoka Yemen na Uhabeshi; jeshi ambalo halina mfano wake. Walipoukaribia Makkah – Waarabu hawakuwa na namna ya kukabiliana na jeshi hili – hapo Allah akawatumia ndege waliotapakaa wakiwa wamebeba mawe kutoka kwa moto. Wakaangushia mawe yale, yakakata miili ya kila aliyekuwepo kwenye jeshi lile, wakaganda na kuduwaa wakawa kama majani yaliyotafunwa yakatemwa. Na Allah akaizuia shari yao na kuwaadhibu kwa lengo lao bovu. Na kisa chao ni maarufu. Kilitokea mwaka ambao ndani yake alizaliwa Mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake. Ikawa ni miongoni mwa mafunzo katika kulingania wale wenye malengo mabaya dhidi ya dini ya Allah.

[TAFSIRI YA SURATU QUREISH]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Li-iilaafi Quraish . (2). Ilaafihim rihlata sh-shitaai wa sswaiif. (3). Falya 'budu u rabba haadhal baiit (4). Alladhii atw-amahum min juuin wa aamanahum min khauuf

(Aya 1-4): Wanasema wengi katika wanazuoni wa tafsiri: Allah aliangamiza jeshi la watu wa ndovu kwa sababu ya Qureish; amani yao na kuendeleza maslahi yao na nidhamu za safari zao kuenda Yemen msimu wa joto na kuenda ukanda wa Syria msimu wa baridi kwa lengo la kibiashara na kuchuma.

Basi Allah akawaangamiza waliowatakia shari na akaitakasa Nyumba Yake tukufu na kuiathimisha kwenye nyoyo zao. Ndio maana Allah akawaamrisha kumshukuru na kumpwekesha Allah kwenye ibada; Mola ambaye anawaruzuku kutokana na njaa na kuwaepusha na hofu. Kuepushwa kutokana na njaa na hofu ndio neema kubwa zaidi katika neema za dunia. Basi hatuna budi kumshukuru Allah kwa neema Zake zilizo wazi na zilizofichika.

[TAFSIRI YA SURATUL MAA^UUN]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). *Ara-aita lladhii yukadh-dhibu biddeen .* (2). *Fadhaalika lladhii yadu^ul yatiim..* (3).
Wa laa yahudh-dhu alaa twa-aamil miskiin. (4). *Fawailul lilmuswalliin.* (5).
Alladhiina hum an swalaatihim saahuun. (6). *Alladhiina hum yuraa-uun.* (7). *Wa
yamnuunal maa^uun.*

(Aya 1): Anasema Allah huku akimkemea yule asiyetekeleza haki Zake na haki za waja *ara-aita lladhii yukadh-dhibu biddeen* (Je. **Umemwona anayekadhibisha malipo**); katika mambo ya kufufuliwa, hesabu, malipo na yale waliyokuja nayo Mitume.

(Aya 2): *Fadhaalika lladhii yadu^ul yatiim* (**huyo ndiye anayemsukuma yatima**) kwa kumfukuza kwa ukali bila kumhurumia. Hii ni kutokana na ugumu wa moyo kwa sababu hatarajii thawabu wala haogopi adhabu ya Kiyama.

(Aya 3): *Wa laa yahudh-dhu alaa twa-aamil miskiin* (**wala hahimizi kumlisha maskini**) na wala haihusii nafsi yake kutenda hilo.

(Aya 4-5): *Fawailul lilmuswalliin* (**basi ole wao wanaosali**) wale wanaopaswa kuhifadhi sala zao lakini wao *an swalaatihim saahuun* (**wanapuuza sala zao**) wamezipoteza, wamezichelewesha kutoka kwa muda wake na wakachelea katika kutimiza nguzo zake na mafunzo yake. Hili ni kutokana na kutozingatia maamrisha ya Allah. Kwa hiyo wakaipoteza sala ambayo ni ibada kubwa sana katika ibada za kimwili. Hawa watapata lawama na adhabu kali siku ya Kiyama.

(Aya 6-7): Allah amewasifu watu hawa kwa sifa ya kujionyesha katika ibada zao, ugumu wa moyo na kutokuwa na huruma kwa kauli yake *alladhiina hum yuraa-uun* (**ambao wanajionyesha**) katika ibada zao *wa yamnuunal maa^uun* (**na huku wanazuia msaada**); hawatoi chochote kile katika njia ya msaada wala zawadi wala mkopo. Hata vitu duni kama chumvi hawatoi kamwe.

Katika surah hii, Allah amehusia kuwalisha maskini, kuhusiana katika kulisha maskini, kusimamisha pamoja na kuhifadhi sala, kumpwekesha Allah katika ibada na kutojionyesha, kutenda mema na kusaidiana katika vitu vya haja na dharura.

[TAFSIRI YA SURATUL KAUTHAR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Innaa a'twainaakal kauthar . (2). Faswalli lirabbika wan-har. (3). Inna shaaniaka huwal abtar.

(Aya 1): Anasema Allah kumwabia Mtume Wake na kumkubusha neema Zake juu yake *innaa a'twainaakal kauthar* (**hakika tumekupa kheri nyingi**) na fadhila nyingi. Na katika kheri atakazompa siku ya Kiyama ni mto unaoitwa Kauthar: urefu wake ni mwendo wa mwezi mzima, upana wake ni mwendo wa mwezi mzima pia, maji yake ni meupe kushinda maziwa, matamu kushinda asali na vyombo vyake vya kunywea ni vingi mfano wa nyota angani. Atakayekunywa kutoka kwenye mto huo hatopata kiu kamwe.

(Aya 2): Na baada ya Allah kumtajia kheri na fadhila hizo, alimuamrisha kushukuru kwa kauli Yake *faswalli lirabbika wan-har* (**basi Sali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi**). Allah alizitaja hizi ibada mbili kwa sababu ndizo ibada bora na kurhani bora; kwa sababu sala inapatikana ndani yake utulivu na unyenyekevu wa moyo na viungo na kuchinja kunapatikana ndani yake kujikurubisha kwa Allah kwa kitu bora anachokimiliki mwanadamu na kujiepusha na uroho na ubakhili.

(Aya 3): *Inna shaaniaka* (**hakika anayekuchukia**) na anayekukemea *huwal abtar* (**ndiye aliye mpungufu**) yaani amezuiliwa na kheri zote kwa kumchukia mbora wa viumbe ambaye amekamilika katika kumuabudu Mola wake.

[TAFSIRI YA SURATUL KAAFIRUUN]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Qul yaa ayyuhal kaafiruun . (2). Laa a'budu maa ta'buduun. (3). Wa laa antum aabiduuna maa a'budu. (4). Wa laa ana aabidum maa abadtum. (5). Wa laa antum aabiduuna maa a'budu. (6). Lakum diinukum wa liya diin

(Aya 1-6): Waambie makafiri kwa bayana kuwa *laa a'budu maa ta'buduun* (**siabudu mnachokiabuudu**) ili kujiepusha na ibada zenu fiche na za dhahiri *wa laa antum aabiduuna maa a'budu* (**wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu**) kwa kutompwekesha Allah katika ibada zenu. Kumuabudu kwenu pamoja na kumshirikisha na miungu mingine hakuitwi ibada.

Basi Allah akatenganisha baina ya vikundi hivi viwili kwa kauli Yake *lakun diinukum wa liya diin* (**nyinyi mna dini yenu na mimi nina dini yangu**).

[TAFSIRI YA SURATU NNASR]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Madinah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Idhaa jaa-a nasrullaahi wal fat-h . (2). Wa-ra-aita nnaasa yadkhuluuna fii diinillaahi afwaaajaa. (3). Fasabbih bihamdi rabbika wastaghfirhu, innahu kaana tawwaabaa.

(Aya 1-3): katika surah hii tukufu, kuna bishara, maamrisho kwa Mtume bishara likitimia, ishara na tanbihi kwa matokea ya hayo.

BISHARA: ni bishara ya nusra ya Allah kwa Mtume Wake na kufunguliwa kwa Makkah, na watu kuingia *fii diinillaahi afwaaajaa* (**katika dini ya Allah kwa makundi**); watakuwa wengi sana katika waliozaliwa na waliosilimu baada ya kuwa maadui wa dini hii.

AMRI BISHARA IKITIMIA: Allah amemuamrisha Mtume Wake wakati bishara itatimia, azidishe shukrani, kusabihi na kumhidi Allah kwa neema hiyo.

ISHARA: hakika kutimia kwa bishara kunaashiria mambo mawili: (1) Nusra ya allah kwa dini itaendelea kwa kusabihi, kuhimidi na kuomba msamaha na kushukuru kwa wingi. Allah anasema, “*la-in shakartum la-aziidannakum*” (**Mkinishukuru nitawazidishieni**). Na hili lilitimia katika zama za makhalifa walioongoka na waliokuja baada yao katika ummah. Na hii nusra iliendelea hadi Uislamu ukafika pembe zote za dunia. Na ikaisha pindi ummah ulipoacha kutii maamrisho ya Allah na kutengana. Lakini nusra na kuhifadhi dini bado Allah amedhibiti. (2) Inaashiria kuwa kifo chake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kilikuwa kimewadia. Kwa sababu katika Sunnah ya Allah ni kuwa hakuna kinachodumu katika walimwengu. Basi akaamrisha kuhitimisha maisha yake kwa Sala na Hijja.

[TAFSIRI YA SURATUL MASAD]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Tabbat yadaa abii lahabin wa tabba . (2). Maa aghnaa anhu maaluhu wa maa kasaba (3). Sayaslaa naaran dhaata lahab. (4). Wamra'tuhu hammaalatal hatwab. (5). Fii jiidihaa hablun min masad.

Abu Lahab alikuwa ni ami yake Mtume. Na alikuwa mwenye maudhi na uadui mkubwa sana dhidi ya Uislamu na Waislamu; wala hakujali kuwa anahusiana na mtume kifamilia na ukoo. Basi Allah akamdunisha na kumdhalilisha hadi siku ya Kiyama kwa kusema: imeangamia mikono ya abu Lahab na kuzorota. Ambaye alikuwa akidhani kuwa mali aliyokuwa nayo itamnusuru siku ya Kiyama. Hakika ataingia jahanamu yeye na mkewe ambaye alishirikiana naye katika kumuudhi Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. Basi Allah akasema wataingizwa motoni yeye na mkewe ambaye atafungwa kamba shingoni kwa madhambi yake ambayo yatakuwa yamemzonga kama mbeba kuni.

[TAFSIRI YA SURATUL IKHLAAS]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

*(1). Qul huwa Allahu ahad . (2). Allahu sswamad. (3). Lam yalid wa lam yuulad.
(4). Wa lam yakun lahu kufuwan ahad*

(Aya 1): Waambie kwa kuamini na kuitikadi *huwa allahu ahad* (**Yeye Allah ni wa pekee**) ametukuka na anayepwekeshwa kwa kila kitu.

(Aya 2): *Allahu sswamad* (**Allah Mkusudiwa**) anayekusudiwa na kulengwa kwa mambo yote na haja zote za waja.

(Aya 3): Na katika ukamilifu wa sifa Zake *lam yalid wa lam yuulad* (**hakuzaa wala hakuzawa**) kwa sababu amejitosheleza.

(Aya 4): *Wa lam yakun lahu kufuwan ahad* (**wala hana anayefanana naye hata mmoja**) Katika majina yake, sifa Zake na katika vitendo Vyake. Ametukuka Allah.

Surah hii imekusanya Tauhidi ya kumpwekesha Allah katika majina Yake na sifa Zake.

[TAFSIRI YA SURATUL FALAQ]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Qul a-uudhu birabbil falaq . (2). Min sharri maa khalaq(3). Wa min sharri ghaasiqin idhaa waqab. (4). Wa min sharri nnaffaathaati fil uqad. (5). Wa min sharri haasidin idhaa hasad.

(Aya 1): Waambie kwa kujilinda kwa Allah *a-uudhu* (**najikinga**) na kujilinda kwa Mola wa mapambazuko.

(Aya 2): *Min sharri maa khalaq* (**na shari ya alivyoviumba**); hii inakusanya viumbe wote; majini, watu na wanyama. Lazima mwanadamu ajilinde kutokana na shari za viumbe hawa.

(Aya 3): *Wa min sharri ghaasiqin idhaa waqaba* (**na shari la giza la usiku liingiapo**) kwa sababu usiku unapowagubikka watu, roho na wanyama wabaya hupatikana kwa wingi.

(Aya 4): *Wa min sharri nnaffaathaati fil uqad* (**na shari ya wanaopulizia mafundoni**); shari za wachawi wanaopuliza kwenye mafundo yao ili kutekeleza uchawi wao.

(Aya 5): *Wa min sharri haasidin idhaa hasada* (**na shari ya hasidi anapohusudu**); Uhasidi ni kule kumtakia ndugu yako neema aliyonayo imwondokee kwa kila namna. Basi mwanadamu anahitaji kinga kutokana na shari hizi zote.

Surah hii imefunza kinga kutokana na aina zote za sharri ikiwemo uchawi na uhasidi.

[TAFSIRI YA SURATU NNAAS]

[Nayo ni surah iliyoshuka msimu wa Makkah]

Bismillahi Rahmani Rahiim

(1). Qul a-uudhu birabbi nnaas. (2). Maliki nnaas(3). Ilaahi nnaas. (4). Min sharril waswaasil khannaas. (5). Alladhii yuwaswisu fii sudduri nnaas. (6). Minal jinnati wa nnaas..

(Aya 1-6): Surah hii inafunza kutafta kinga kwa Allah kutokana na shari za shetani na fitina zake. Ambaye shetani huyu, sifa yake ni *yuwaswisu fii suddri nnaas* (**anayetia wasiwasi katika vifua vya watu**) kwa kuwapendzeshea shari na kuwapambia maovu na kuwahamasisha kutekeleza maovu yale. Kisha Allah akaelezea kuwa mashetani ni aina mbili; *minal jinnati wa nnaas* (**kutokamana na majini na wanadamu**)

Tunamshukuru Allah kwa kutujaalia kuikamilsha tafsiri ya baadhi ya surah za Kur’ani. Kisha rehema na amani zimwendee Mtume Wake.

MASUALI YA SURATUL FIIL

1. Surah hii ilishuka msimu wa Makkah au Madinah?
2. Ndani ya Surah hii, Allah ametaja uhatari wa kuifanyia uadui nyumba Yake. (sahihi / sio sahihi)
3. Alizaliwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, mwaka wa

☐ Ndovu
☐ Huzuni
☐ Ukame
4. Allah aliwaadhibu jeshi kwa
5. Kila aliyepatwa na jiwe, alikuwa kama

MASUALI YA SURATU QUREISH

6. Surah hii ilishuka msimu wa Makkah au Madinah?
7. Hii surah ina uhusiano na surah ipi?

☐ Al-Fiil
☐ Kaafiruun
☐ An-Naas
8. Qureish walikuwa wakisafiri kwenda msimu wa joto na msimu wa baridi.

MASUALI YA SURATUL MAA^UUN

9. Surah hii ilishuka msimu wa.....
10. Kuikadhibisha dini inamaanisha

☐ Kufufuliwa na malipo
☐ Kukanusha madeni ya watu
11. *Yadu^u* inamaanisha

☐ Kumwacha
☐ Kumfukuza na kumkataza kwa ukali
12. Yatima ni yule ambaye amefiwa na kabla ya kubaleghe.
13. Ni kusahau kupi kunahatarisha imani?

14. Hukumu ya kutenda jambo kwa kujionyesha

☐ Inaruhusiwa
☐ Imeharamishwa
15. Katika surah hii Allah amehusia baadhi ya mambo, kwa mfano

-
 -
 -
 -
 -

16. Maa^uun inamaanisha

MASUALI YA SURATUL KAUTHAR

17. Surah hii ilishuka msimu wa

18. Al-Kauthar ni

☐ Mto

☐ Kheri na fadhila nyingi

19. Allah alitaja hizi ibada mbili: na kwa sababu ndio ibada bora zaidi.

20. *Shaaniaka* inamaanisha

☐ Anayekuchukia

☐ Anayekudhalilisha

☐ Yote mawili ni sahihi

21. Surah hii imefunza kuwa kumpeda Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuna ondoa hasara. (sahihi / sio sahihi)

22. Je, kwenye surah hii kuna dalili kuwa watakaonusuru dini watakuwa wengi?

MASUALI YA SURATUL KAAFIRUUN

23. Surah hii ilishuka msimu wa

24. Surah hii inasomwa katika rakaa ya kwanza baada ya suratul Fatihah katika swala ya

☐ Sunnah ya Alfajr

☐ Sunnah ya Maghrib

☐ Sunnah ya Twawaaf

☐ Witri

☐ Sala zote ziizotajwa

25. Ibada iliyochanganyika na shirki ni ibada (kamili/pungufu)?

26. Kafiri ni nani?

☐ Kila aliyefikiwa na wito wa Uislamu na hakuamini

☐ Watu wa Makkah pekee waliokataa Uislamu

MASUALI YA SURATU NNASRI

27. Surah hii ilishuka msimu wa

28. Surah hii ndani yake kuna bishara, amri na ishara. (sahihi / sio sahihi)

29. Je, ndani ya surah hii kuna ishara ya kukaribia kifo chake, rehema na amani ziwe juu yake?

MASUALI YA SURATUL MASAD

30. Surah hii ilishuka msimu wa

31. Abu Lahab alikuwa ni yake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.
32. Elezea maana ya maneno haya
Tabbat:
Maa kasaba:
Jiidihaa:
Masad:
33. Ndani ya surah hii kuna dalili kuwa Abu Lahab na mkewe hawataasilimu. (sahihi / sio sahihi)

MASUALI YA SURATUL IKHLAAS

34. Surah hii ilishuka msimu wa
35. Mbona surah hii imeitwa kwa jina la *Ikhlaas*?
36. Surah hii kuisoma ni sawa na kusoma ya Kur'ani.
- ☐ Robo
 - ☐ Thuluthi
 - ☐ Nusu
37. Surah inasomwa katika rakaa ya pili baada ya Fatihah katika swala gani?
- ☐ Sunnah ya Alfajr
 - ☐ Sunnah ya Maghrib
 - ☐ Sunnah ya Twawaaf
 - ☐ Witri
 - ☐ Baada ya swala za faradhi
 - ☐ Yote ni sahihi
38. Surah hii imetaja aina gani ya Tauhidi?
39. Kumsingizia Allah mtoto ni
- ☐ Kufu kubwa
 - ☐ Shiriki ndogo

MASUALI YA SURATUL FALAQ

40. Surah hii ilishuka msimu wa
41. Surah hii inasomwa wakati gani?
- ☐ Baada ya sala za faradhi
 - ☐ Wakati wa kulala
 - ☐ Nyakati zote mbili
42. Elezea maana na maneno haya:

Audhu:

Alfalaq:

Ghaasiq:

Waqab:

Haasid:

43. Surah hii inafunza kujikinga kutokana na kila kitu. (sahihi / sio sahihi)

MASUALI YA SURATU NNAAS

44. Surah hii ilishuka msimu wa

45. Inasomwa surah hii

☐ Baada ya sala za faradhi

☐ Wakati wa kulala

☐ Nyakati zote mbili

46. Wanaotia wasiwasi ni na

SOMO LA PILI

SOMO LA PILI: NGUZO ZA UISLAMU

Kubainisha nguzo tano za Uislamu; ya kwanza ni kushuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mtume Wake, kubainisha masharti ya shahada na kueleza maana ya baadhi ya maneno katika shahada.

Masharti ya Shahada ni:-

1. Elimu inayokanusha ujahili
2. Yakini inayokanusha shaka
3. Ikhlaas inayokanusha shirki
4. Ukweli unaokanusha kukadhibisha
5. Mapenzi yanayokanusha chuki
6. Utekelezaji unaokanusha utotekelezi
7. Kukubali kunakokanusha kupinga
8. Kuikufuru miungu yote inayoabudiwa kando na Allah.

Pia tutabainisha shahada ya kuwa Muhammad ni mtume Wake pamoja na masharti yake.

Kisha tutabainisha nguzo za Uislamu zilizobaki.

NGUZO ZA LAI ILAAHA ILA

KUKANUSHA

Kuikanusha miungu yote inayoabudiwa

KUTHIBITISHA

Kumthibitishia ibada zote Allah na kumpwekesha katika ibada zote

MASHARTI YA SHAHADA (LAI ILAAHA ILA ALLAH)

Umuhimu wa masharti ya shahada ni sawa na umuhimu wa meno kwenye ufunguo. Shahada ni ufunguo wa jannah na kama ilivyo kawaida ni kuwa ufunguo usiokuwa na meno hauwezi kuufungua. Na bishara njema zilizokuja kuelezea umuhimu wa shahada, hakika haziwezi kutimia mpaka kupatikane masharti haya manane:- ambayo ni

- 1. ELIMU:** elimu iliyokamilika na kinyume chake ni ujahili. Asiyejua maana ya shahada basi shahada hii haitomfaa chochote. Inamlazimu kila anayetaka kuingia katika Uislamu aifahamu maana ya shahada (Lai ilaaha ila Allah). Anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“Atakayekufa huku akifahamu kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, ataingia jannah.”* (Ameipokea Muslim)
- 2. YAKINI:** awe na yakini asilimia 100. Hakika ya shaka hata kama ni asilimia moja katika shahada au kupata wasiwasi katika shahada inamtoa mtu katika duara la Tauhidi. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“Nashuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hakika mimi ni mtume Wake. Yeyote atakayekutana na Allah akishuhudia haya mawili pasina kuwa na shaka basi ataingia jannah.”* (Ameipokea Muslim)
- 3. IKHLAAS:** kumpwekesha Allah ni wajibu. Atakayejiionesha katika ibada au kumshirikisha Allah na chochote katika ibada kwa mfano kuabudu sanamu, ibada hiyo haitomfaa kamwe. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“Aliye bora zaidi kwa maombezi yangu siku ya Kiyama ni yule atakayetamka: Lai ilaaha ila Allah kwa ikhlaas kutoka moyoni mwake au kutoka kwa nafsi yake.”* (Ameipokea Bukhari)
- 4. UKWELI:** Atakayetamka shahada kwa uongo – kama mnafiki – haitomfaa shahada hii, amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“Hakuna yeyote anayeshuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kuwa Muhammad ni mja Wake na mtume Wake kwa ukweli kutoka moyoni mwake isipokuwa mtu huyu Allah atamharamishia moto.”* (Ameipokea Muslim)
- 5. MAPENZI:** Ampende Allah pekee wala asikipende pamoja na Allah chochote kile. Na ampende kila aliyeamrisha Allah kumpenda. Na kinyume chake ni chuki; ndio maana

ikawa kuchukia chochote alichokuja nacho Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kunamtoa Uislamuni hata kama atakifanyia kazi. Amesema Allah, “*Na miongoni mwa watu kuna wale wanaoifanya miungu na wakaipenda kama wanavyompenda Allah.*”

6. **UTEKELEZAJI:** Lazima kuifanyia kazi shahada. Yeyote ambaye hatoifanyia kazi shahada haitomfaa, amesema Allah, “*Hakika kwa haki naapa kwa Mola wako Mlezi. Hawatokuwa wenye kuamini hadi wakufanye hakimu kwa ugomvi unaotokea baina yao kisha wasipate moyoni dosari katika hukumu yako na waikubali kwa ukamilifu hukumu yako.*”
7. **KUIKUBALI:** asiipinge shahada kwa maneno, vitendo au itikadi, anasema Allah, “*Hakika wao walikuwa wakiambiwa: hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, wanafanya kiburi huku wakisema: Haiwezekani sisi kuiacha miungu yetu kwa maneno ya mshairi wazimu.*”
8. **KUIKUFURU MIUNGU:** Lazima aikufuru ibada ya miungu inayoabudiwa kando na Allah na azipwekeshe ibada zote kwa Allah pekee.

TANBIHI

LAZIMA MTU ATIMIZE MASHARTI HAYA KWA MANENO, VITENDO NA ITIKADI.

AINA ZA MAPENZI

MAPENZI PAMOJA NA ALLAH

Na hii ni shirki kubwa. Amesema Allah, “*Na miongoni mwa watu, kuna wale wanaopenda miungu kama mapenzi yao kwa Allah*”

KUMPENDA ALLAH

Na hii ni wajibu kwa kila mja bali ni moja katika shina kuu za imani. Amesema Allah, “*Muhammad ni mtume wa Allah. Na wale walioko naye ni wakali kwa makafiri na rahimu baina yao*”
Mapenzi haya yanakuwa katika mambo manne:-

MAPENZI YA KIMAUMBILE

Na hii imeruhusiwa kwa sharti: isipite mapenzi ya kumpenda Allah. Mfano wake: kumpenda mtoto au mke. Amesema Mtume, “*Hatoamini mmoja wenu mpaka anipende zaidi ya mwanawe, mzazi wake na watu wote.*”

KITENDO

Kitendo anachokiridhia Allah: nayo ni kila kilichokuja katika sharia kwa mfano Tauhidi

MTENDEA KAZI

Kama Manabii, Mitume, Malaika, Masahaba na kila anayempwekesha Allah.

ZAMA/MUDA

Zama/muda anaoupenda Allah kwa mfano Leilatul Qadri na thuluthi ya mwisho ya usiku.

SEHEMU

Sehemu anazopenda Allah kama miji ya Makkah na Madinah yake Mtume.

MAANA YA MJA KATIKA SHAHADA INAYOSEMA: MUHAMMAD NI MJA WAKE NA MTUME WAKE

Haabudiwi kwa sababu yeye hana sifa yoyote katika uungu, mola wala pia hana sifa za ukamilifu kama za Allah.

Yeye ndiye mbora wa viumbe katika kumuabudu Allah basi anakuwa ametimiza sifa kamili ya kufanya ibada.

AINA ZA KUABUDU

JUMLA

Hii ni ibada ya ulezi wa viumbe (kumiliki na kuendesha) na kila kiumbe kinamnyenyekea katika hali hii. Allah anasema, “*Na hakika. Kila aliye mbinguni na ardhini atamjia Allah siku ya Kiyama akiwa mja*” Katika hii, anaingia Muumini na kafiri

HASA

Hii ni ibada ya kumcha Mwenyezi Mungu kijumla. Amesema Allah, “*Na waja wa Mwenyezi Mungu ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu*” Na ibada hii ni kwa kila aliyemfuata Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, katika mafunzo yake.

MAALUM

Hii ni ibada ya Mitume. Amesema Allah, “*Hakika alikuwa ni mja mwenye kushukuru.*” Na hii ilikuwa ibada maalum kwa Mitume kwa sababu hakuna anayewashinda Mitume katika kumuabudu Allah.

MUKHTASAR WA HISTORIA YA MTUME MUHAMMAD, REHEMA NA AMANI ZIMWENDEE

NASABA YAKE

Muhammad bin Abdillahi bin Abdilmuttalib bin Hashim. Na Hashim ni kutoka kwa Qureish. Na Qureish ni kutoka kwa Waarabu. Na Waarabu ni katika kizazi cha Ismail bin Ibrahim, Allah awape salama.

KUZALIWA KWAKE

Alizaliwa mwaka wa ndovu kwenye mji wa Makkah mwezi wa tatu. Aliishi miaka sitini na mitatu (63); arbaini kabla ya unabii na ishirini na mitatu akiwa nabii mtume. Alizaliwa yatima; baba yake alifariki kabla ya kuzaliwa kwake; basi akawa katika malezi ya babu yake Abdulmuttalib na alipokufa babu yake, ami yake Abu Twalib ndiye alichukua majukumu ya kumlea.

WALIOMNYONYESHA

1. Mamake Amina bint Wahb
2. Thuwaibah, mjakazi wa ami yake Abu Lahab
3. Halima bint Abu Duwaib As-Saadiyyah

UTUME

Alitumwa kwa ajili ya viumbe wote; majini na wanadamu. Kila aliyefikiwa na wito wake na akafa bila ya kumuamini basi amekufa katika ukafiri.

WITO WAKE	Aliwalingania watu kwenye kumpwekesha Allah katika ibada Yake, tabia njema na akakataza ushirikina na tabia mbovu.
SAFARI YA ISRAA NA MI'RAJ	Allah alimsafirisha usiku kutoka Makkah hadi msikiti wa Aqsa kisha akamnyanyua hadi mbingu ya saba, akamzungumzisha kisha akamfaradhisia sala tano.
KUGHURA NA KIFO	Alighura kutoka mji wa Makkah kwenda mji wa Madinah. Na katika mji wa Madinah alifariki dunia na akazikwa humo; ndani ya chumba cha mkewe Aisha, Allah awe radhi naye.
KULINGANIA KWAKE	Allah alimkamilishia dini. Na yeye akalingania kiukamilifu kwa dini ya Allah, akatekeleza amana ya utume aliyopewa, akanasihi ummah, akapambana kwa njia ya Allah kwa kila namna; haiwezekani yeyote kuzidisha chochote katika dini hii.
VITA VYAKE MUHIMU	1. Badri 2. Uhud 3. Khandaq 4. Khaibar 5. Ufunguzi wa Makkah 6. Tabuk 7. Hunein
WATOTO WAKE SABA	- Qassim - Ibrahim - Abdullahi - Zeinab - Ruqaiyah - Ummu Kulthum - Fatuma Wote walikufa akiwa hai isipokuwa Fatuma aliyefariki miezi sita baada ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.

WAKE
ZAKE

1. Khadija
2. Aisha
3. Sauda
4. Hafsa
5. Zeinab kutoka kabila la Hilal
6. Ummu Salama (Hind)
7. Zeinab bint Jahsh
8. Juweiriya bint Harith
9. Sofia bint Huyeiy
10. Ummu Habiba (Ramla)
11. Rihana bint Zeid
12. Maimuna bint Harith

UFUNUO
WA
KWANZA
ALIOPEWA

Aya tano za mwanzo katika Suratul [^]Alaq
(Surah nambari 96 katika Kur'ani)

WALIOMWANI
MWANZO

1. Katika wanaume : *Abubakar Siddiq*
2. Katika wanawake : *Mkewe Khadija*
3. Katika watoto : *Binamu yake (Ali bin Abi Twalib)*
4. Katika wajakazi : *Zeid bin Harith*
5. Katika watumwa : *Bilal bin Rabah*

HIJJA ZAKE
NA UMRAH

Alifanya umrah nne, zote alikuwa anazifanya katika mwezi wa kumi na moja (Dhul Qaadah) na alifanya Hijja moja katika umri wake; inaitwa Hijja ya kuaga iliyofanyika mwaka wa 10 Hijri.

TABIA
YAKE

Allah anamsifu akisema, “*Hakika wewe ni mwema wa tabia*”.
Anasema Aisha, Allah awe radhi naye, “**ilikuwa tabia yake ni Kur'ani.**”

UMUHIMU
WA
KUISOMA
HISTORIA
YAKE

Anasema Ibn Qayyim: *Ikiwa kufaulu duniani na akhera kumefungamanishwa na uongofu wake Mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, ni wajibu kwa kila mmoja anayenasihhi nafsi yake na kuipenda aitambue historia yake, rehema na amani ziwe juu yake, ili apate mazingatio kutoka kwa maisha yake.*

SOMO LA TATU

SOMO LA TATU: NGUZO ZA IMANI

Nguzo za Imani ni sita: Kumwamini Allah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Kiyama na kuamini Qadar Yake; kheri yake na shari yake.

MAANA YA IMANI

Kutamka kwa ulimi, kukiri kwa moyo na kutenda kwa kiwiliwili na viungo. – imani huzidi na kupungua.

Dalili ya KUTAMKA KWA ULIMI

Hadith, “*Tawi la juu katika imani ni kutamka: Laa ilaaha illa Allah*”

Dalili ya KUTENDA KWA KIWILIWILI

Hadith, “*Tawi la chini katika imani ni kuondoa maudhi barabarani*”

Dalili ya KUTENDA KWA MOYO

Hadith, “*Na kuwa na haya ni katika matawi ya imani*”

Dalili ya KUZIDI IMANI

Aya, “*Ni yupi kati yenu hili lilimzidisha imani*”

Dalili ya KUPUNGUA IMANI

Hadith, “*Sijaona mpungufu wa akili na dini kama mwanamke...*”

SABABU ZINAZOMZIDISHIA MTU IMANI


Kuisoma Tauhidi hasa mlango wa Majina na Sifa za Allah.

Kuzidisha mambo ya ucha Mungu


Kuacha maasi na dhambi

Kutafakari katika maumbile ya Allah.


SABABU ZINAZOPUNGUZA IMANI YA MJA



NGUZO SITA ZA IMANI



NGUZO YA KWANZA YA IMANI: KUMUAMINI ALLAH



NGUZO YA PILI YA IMANI: KUAMINI MALAIKA WAKE

Malaika ni viumbe katika ulimwengu wa ghaibu. Allah amewaumba kwa nuru, wanamtii Allah na wala hawakiuki amri Zake. Wana nafsi kama alivyowasifu Allah kwa kauli Yake, *“Roho mtakatifu”*, wana mwili kama alivyosema, *“Ametukuka aliyewaumba malaika na kuwafanya mitume wenye mbawa mbili-mbili, tatu-tatu, nne-nne, huzidisha katika uumbaji Wake anachokitaka.”* Wana akili na nyoyo. Malaika hawa tunawaamini kwa yale alotupa elimu Allah katika majina yao kama Jibril, Mikail na Israil, na katika sifa zao kama, *“Hawamuasi Allah anachowaamrisha na wao hutekeleza wanayoamrisha.”* Na katika kazi zao.

BAADHI YA MALAIKA TULIOTAJIWA

Kuna Wabeba Arshi wanane, Jibril ambaye ni mhusika wa kushuka na ufunuo, Mikail ambaye ni mhusika wa hali ya anga na hewa. Tunawaamini wote na yote yaliyotajwa kuwahusu kwa ufupi na upana, kijumla na ufafanuzi.

NGUZO YA TATU YA IMANI: KUAMINI VITABU VYAKE

Ni lazima tuamini kuwa haya ni maneno ya Allah kiuhakika bila ya majazi na kuwa viliteremshwa wala havikuumbwa. Na lazima kuamini pia kuwa kila Mtume, Allah alimteremshia kitabu na tunaviamini kama alivyoelezea Allah kuhusu habari zao, majina yao na hukumu zao kijumla na ufafanuzi. Na pia tuamini kuwa Kur’ani ilishuka ikafuta vitabu vya awali kama Torati, Zaburi, Injili na nyaraka za Ibrahim na Musa.

NGUZO YA NNE YA IMANI: KUWAAMINI MITUME WAKE

Ni lazima tuamini kuwa Mitume ni viumbe ambao hawana sifa katika uungu na kuwa Mitume hawa ni waja wala hawapaswi kuabudiwa. Na tuamini kuwa Allah aliwatumiliza, akawapa ufunuo, akawapa miujiza ya kusadikisha wasemayo, na tuamini kuwa Mitume hawa walitekeleza amana ya utume, wakanasihi ummah, wakalingania na kueneza risala pamoja na kupambana katika njia ya Allah kuhakikisha mapenzi ya Allah yanatekelezwa.

Tunawaamini, na aliyotuelimisha Allah kuhusu sifa zao, habari zao na majina yao. Nabii wa kwanza alikuwa ni Adam na mtume wa kwanza alikuwa ni Noah na wa mwisho katika Manabii na Mitume alikuwa ni Muhammad, rehema na amani ziwe juu yao wote. Tunaamini pia kuwa sheria alokuja nayo mtume Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake, ilifuta sheria zilizotangulia.

Na miongoni mwa Mitume, kuna wale Allah aliwanyanyua daraja zaidi ya waliobaki, nao ni Muhammad, Noah, Ibrahim, Musa na Isa, Allah awape salama.

NGUZO YA TANO YA IMANI: KUIAMINI SIKU YA MWISHO

Nguzo hii inamaanisha kuamini kila alichoelezea Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuhusu yale yatakayotokea baada ya kifo; kama mitihani ya kaburini, kupulizwa baraghumu, kufufuliwa watu, kupimwa vitendo katika mizani, kupewa kitabu cha matendo, kupita njia ya swiraat, kisima cha Mtume, maombezi, jannah, jahanamu, waumini kumuona Allah siku ya Kiyama na mengine mengi.

NGUZO YA SITA YA IMANI: KUIAMINI QADAR YAKE

Qadar ni mipangilio Yake Allah katika uumbaji. Na Qadar ina hatua nne:-

ELIMU

Tunaamini kuwa Allah alikijua kila kitu kwa upana kabla ya kuumba. Dalili ya hayo ni aya, “*Anajua yaliyokuwa kabla yao na yatakayokuwa kwenye mustakbali wao*”

UANDISHI

Tunaamini kuwa Allah, kabla ya kuumba, aliandika mipangilio ya kila kitu hadi siku ya Kiyama. Dalili ya hayo ni aya, “*Hakuna kilichofichika mbinguni wala ardhini isipokuwa kiko katika maandishi yaliyo wazi.*”

MATAKWA

Tunaamini kuwa kila alichokitaka Allah kinakuwa, na kila asichokitaka hakiwi, na kuwa mja pia kapewa matakwa yaliyo chini ya matakwa ya Allah. Anasema, “*Na wala hamtaki isipokuwa alichokitaka Allah.*”

UUMBAJI

Tunaamini kuwa mja ni kiumbe na vitendo vyake pia vimeumbwa, na vilivyomo vyote vimeumbwa. Anasema Allah, “*Allah ni muumbaji wa vyote*” “*Na Allah amewaumbeni na mtendavyo.*”

SOMO LA NNE

AINA ZA TAUHIDI NA AINA ZA SHIRKI

Kubainisha aina tatu za Tauhidi: kumpwekesha Allah katika Malezi, kumpwekesha Allah katika ibada na kumpwekesha Allah katika majina na sifa Zake:-

- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA MALEZI:** ni kuamini kuwa Allah ndiye muumbaji wa vitu vyote na mwendesaji wa kila kitu na wala hana mshirika katika hayo.
- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA IBADA:** ni kuamini kuwa Allah ndiye apasaye kuabudiwa kwa haki na hana mshirika katika ibada. Na hii ndio maana halisi ya shahada. Ibada zote; swala, saum na zingine, anastahiki kupwekeshwa nayo Allah pekee na haifai kuielekeza ibada hiyo kwa miungu mingine.
- **KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA MAJINA NA SIFA ZAKE:** ni kuamini yote yalokuja kwenye Kur’ani na Sunnah kuhusiana na majina na sifa za Allah pasina kubadilisha maana wala kuzikanusha wala kuzitolea namna wala kuzifananisha na chochote katika viumbe. Anasema Allah, “*Hakuna mfano Wake chochote, na hakika Yeye ni mwenye kusikia na mwenye kuona.*”

Na baadhi ya wanazuoni wameigawanya Tauhidi kwa aina mbili; kwa kuingiza kumpwekesha Allah katika majina na sifa Zake katika kumpwekesha kwa ibada.

Shirki imegawanyika aina tatu:- shirki kubwa, ndogo na fiche.

- **SHIRKI KUBWA:** ni ile inayoporomosha amali zote za mja na kumdumisha jahanamu akifa katika hali hiyo, amesema Allah, “*Lau wangemshirikisha Allah na chochote ingeliporomoka amali yao.*” Na amesema pia, “*Haifai kwa washirikina kuitawala misikiti ya Allah hali ya kuwa wanaishuhudia nafsi zao katika ukafiri. Wao ni wale mema yao yameporomoka na ndani ya moto watadumu milele.*” Na atakaye kufa katika shirki kubwa hatosamehewa na ameharamishiwa jannah, asema Allah, “*Hakika ya Allah hamsamehe mwenye kumshirikisha na husamehe madhambi mengine kwa amtakaye*” pia anasema, “*Hakika atakayemshirikisha Allah basi huyo Allah amemharamishia jannah na makaazi yake ni motoni wala hatopata wa kumnusuru.*”

Katika aina za shirki kubwa ni kuabudu maiti na sanamu, kutaka msaada kwao, kuwatolea nadhiri, kuwachinjia na mfano wa hizo.

- **SHIRKI NDOGO:** ni ile iliyotajwa katika Kur’ani au Sunnah kuwa ni shirki

lakini sio katika aina za shirki kubwa, kama kujionyesha katika ibada na kuapa na asiyekuwa Allah na mfano wake. Amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“Kikubwa mno ninachowahofia ni shirki ndogo”* akaulizwa kuihusu akasema, *“Kufanya ibada kwa nia ya kujionyesha kwa watu.”* Na pia katika kauli yake, *“Atakayeapa kwa chochote kando na Allah basi amefanya shirki.”*

Shirki ndogo haimuondoi mtu katika Uislamu wala haitomdumisha mtu motoni akifa katika hali hiyo lakini inakanusha ukamilifu wa imani.

- **SHIRKI FICHE:** anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kuihusu, *“Je. Niwaelezeni ninachowahofieni kwenu zaidi ya masihi dajjal?”* wakasema tueleze ewe Mtume wa Allah, akasema, *“Shirki fiche: ni mtu kusimama katika sala yake kisha akaipamba kwa sababu ya wanaomtizama.”*

Pia shirki inatosheleza tu kugawanywa kwa aina mbili: kubwa na ndogo maana fiche inaingia ndani ya aina zote mbili; kubwa na ndogo.

- Inaingia kwenye Shirki Kubwa kama shirki ya wanafik; kwa sababu wanaficha ukafiri moyoni na wanadhihirisha Uislamu.
- Na inaingia kwenye Shirki Ndogo kama tulivyoona kwenye hadith iliyotangulia.

AINA ZA HARAMU

SHIRKI KUBWA

Ndiyo daraja ya juu katika haramu

SHIRKI NDOGO

Ndiyo inayofuata katika daraja ya pili za haramu

DHAMBI KUBWA

Ni kila dhambi yenye adhabu maalum na imehusishwa na laana na kutengwa mtendaji wake.

DHAMBI NDOGO

Ni kila kilichoharamishwa kisheria pasina adhabu maalum wala kufungamana na laana.

DHAMBI KUBWA

IDADI YAKE

Haina idadi maalum ila ina vidhibiti maalum vilivyotajwa

HUKUMU YA MTENDAJI

- Ni muumini mpugufu wa imani/ muovu kwa dhambi hilo
- Anapendwa kadri ya imani yake na anachukiwa kadri ya uovu wake.
- Haifai kuketi naye wakati wa kutekeleza ovu lile.

TARATIBU ZAKE

Zinatofautiana katika daraja na taratibu. Amesema Mtume, *“Je. Niwaambieni daraja ya juu katika dhambi kubwa”*

HUKUMU YAKE

Ni lazima mja afanye tauba kwa kauli ya Mtume, *“Mpiga mayowe kwa kilio cha maiti asipotubu basi”*

TOFAUTI BAINA YA SHIRKI KUBWA NA SHIRKI NDOGO

SHIRKI KUBWA

1. Inamtoa mtu katika Uislamu
2. Inaporomosha amali zote
3. Inawajibisha mtu kudumu Jahanamu
4. Inahalalisha damu na mali ya mja (hili ni jukumu la kiongozi)
5. Inakuwa kwa dalili kuonyesha kuwa ni kubwa
6. Aitikadi kwenye sababu na kuacha mwenye kuleta sababu
7. Hatosamehewa mtu akifa kwa hali hii
8. Mja akitubu tauba yake inakubaliwa isipokuwa nyakati mbili:-
 - Jua likichomoza kutoka magharibi
 - Wakati wa kufa

SHIRKI NDOGO

1. Haimtoi mtu katika Uislamu
2. Haiporomoshi amali isipokuwa tu ile iliyopatikana ndani yake hiyo shirki
3. Haimdumishi mtu Jahanamu
4. Haihalalishi damu wala mali ya mja
5. Lazima ije dalili kuonyesha kuwa ni ndogo
6. Kuifanya sababu jambo ambalo Allah hajalifanya sababu
7. Kila kinachopelekea shirki kubwa basi hicho kitu ni shirki ndogo

SOMO LA TANO

IHSANI

Nguzo ya Ihsani ni moja: kumuabudu Allah ni kana kwamba unamuona na kama humuoni basi Yeye anakuona.

TABAKA MBILI ZA NGUZO YA IHSANI

IBADA YA USHAHIDI

Hii ni ibada kwa mapenzi kwa Allah. Na ibada hii ni maalum kwa Manabii na Mitume.

IBADA YA UCHUNGAJI

Hii ni ibada ya hofu na uoga ambayo kila Muislamu anakuwa nayo akijua kuwa Allah anatizama kila analolifanya.

MASUALI YA TAUHIDI

1. Daraja za Dini ni ngapi?

- ☐ 3
- ☐ 2
- ☐ 5

2. Nguzo za Uislamu ni ngapi?

- ☐ 5
- ☐ 6
- ☐ 7

3. Uislamu ni daraja la juu kuliko Imani..... (sahihi / sio sahihi)

4. Nguzo za shahada ni ngapi?

- ☐ 7
- ☐ 8
- ☐ 2

5. Masharti ya Shahada ni ngapi?

- ☐ 8
- ☐ 7
- ☐ 5

6. Elimu katika shahada inamaanisha

- ☐ Kuijua uhalisia wa jambo
- ☐ Kujua kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah

7. Kukubali katika masharti ya shahada kunakusudiwa kukubali kwa

- ☐ Maneno
- ☐ Vitendo
- ☐ Itikadi
- ☐ Yote ni sahihi

8. Lau mtu akishuku kuwa Mayahudi ni makafiri. Je mtu huyu ni Muislamu au ametoka?

9. Kujionyesha katika shahada ni sawa na kujionyesha katika shirki ndogo?.....

10. Atakayetamka shahada kwa ulimi pasina kukiri moyoni. Mtu huyu ni

- ☐ Mpwekeshaji
- ☐ Muislamu lakini sio muumini
- ☐ Kafiri ukafiri mkubwa
- ☐ Dhaifu wa imani

11. Lau mtu atampenda Mtume mapenzi sawa na anayompenda Allah. Mtu huyu atakuwa

- ☐ Amekufuru kufr kubwa
- ☐ Amekufuru kufr ndogo
- ☐ Ametenda dhambi katika dhambi kubwa

12. Aina za mapenzi ni ngapi?

- ☐ 4
- ☐ 3
- ☐ 2

13. Kupenda pamoja na Allah ni

- ☐ Shirki ndogo
- ☐ Wajibu
- ☐ Shirki kubwa

14. Aina za kuabudu ni ngapi?

- ☐ 2
- ☐ 3
- ☐ 4

15. Jaza pengo

Alizaliwa Mtume Muhammad mwaka wa Mji wa na aliishi miaka ambayo ni kabla ya utume na katika unabii na utume.

16. Alitumilizwa kwa

- ☐ Kabila lake
- ☐ Watu wote
- ☐ Viumbe wote; majini na wanadamu

17. Alighura kwenda mji wa

- ☐ Uhabeshi
- ☐ Madinah
- ☐ Miji yote miwili ni sahihi

18. Alisafirishwa usiku kutoka kwenda msikiti wa.....

19. Alipigana vita kuu muhimu (1/2/3/4/7)

20. Alikuwa na watoto

21. Alifanya Hijja ngapi katika umri wake?

22. Kusoma historia yake (ni lazima / inapendekezwa / haifai)

23. Nguzo za Imani ni

24. Kumuamini Allah kuna mambo mangapi? (3 / 4 / 5)

25. Dalili za kuonyesha kuwepo kwa Allah ni ngapi? (3/4/ haina idadi)
26. Mikail ni malaika anayehusika na
27. Binadamu wana nyoyo lakini malaika hawana nyoyo..... (sahihi / sio sahihi)
28. Ni vitabu vingapi vilitajwa majina yao?
29. Allah alimshushia kila Mtume kitabu..... (sahihi / sio sahihi)
30. Nabii wa kwanza ni
31. Muhammad ni mtume lakini sio nabii..... (sahihi / sio sahihi)
32. Mitume bora ni wangapi?
33. Kuiamini siku ya mwisho inamaanisha
.....
.....
.....
34. Hatua za Qadar ya Allah ni nne: 1 2.....3.....4.....
35. Je. Allah anajua vitu kabla ya kutokea?.....
36. Je. Kila anachokijua mwanadamu anakijua Allah?.....
37. Je. Kila anachokitenda mwanadamu anakijua Allah?.....
38. Je. Mwanadamu ana matakwa ya kujitegemea?.....
39. Je. Vitendo vya mwanadamu vimeumbwa?.....
40. Je. Tauhidi imegawanyika aina ngapi?.....
41. Taja tofauti tano baina ya shirki kubwa na shirki ndogo.
1
2
3
4
5
42. Toa mifano tano ya shirki kubwa na tano ya shirki ndogo

SHIRKI KUBWA	SHIRKI NDOGO

43. Unafiki wa itikadi unamtoa mtu kwenye Uislamu..... (sahihi / sio sahihi)
44. Ihsani ina nguzo moja. Nayo ni

SOMO LA SITA

MASHARTI YA SALA

Masharti ya Sala ni tisa:-

- | | | |
|-----------------------|---------------------------|------------------|
| 1. Uislamu | 2. Akili timamu | 3. Upambanuzi |
| 4. Kuondoa sifa zuizi | 5. Kuondoa uchafu (najis) | 6. Kusitiri uchi |
| 7. Kuingia muda | 8. Kuelekea Qiblah | 9. Nia |

SHARTI LA KWANZA: UISLAMU

Kinyume chake ni ukafiri. Lau mtu anayemtusi Allah au mshirikina atasali basi sala yake haitokubalika hadi alete tauba ya kikweli.

SHARTI LA PILI: AKILI TIMAMU

Kinyume chake ni wendawazimu au akili punguani. Na ulevi ni zaidi.

SHARTI LA TATU: UPAMBANUZI

Upambanuzi ni tofauti na kubaleghe. Maana ya upambanuzi ni uwezo wa kutofautisha na kupambanua utofauti baina ya vitu; yaani kuelewa suali na jawabu. Na upambanuzi hauna umri maalum lakini mara nyingi mtu katika umri wa miaka saba anakuwa mpambanuzi.

Ni wakati gani inasihi sala ya mtoto mdogo ambaye hajabaleghe? Akiwa na uwezo wa kupambanua baina ya vitu; kwa mfano kutofautisha baina ya maji na moto.

SHARTI LA NNE: KUONDOA SIFA ZUIZI (HADATH)

Sifa zuizi ni sifa ambayo ikipatikana kwa mja inamzuia kutekeleza ibada ya sala.

HADATH KUBWA

(Kama: janaba, hedhi na mengine)

Huondolewa kwa kuoga

HADATH NDOGO

(Kama: kukidhi haja, usingizi na mengine)

Huondolewa kwa kutawadha

SHARTI LA TANO: KUONDOA UCHAFU (NAJIS)

Kuondoa uchafu mwilini, nguoni au kwenye sehemu ya ibada. Lau atasali na najis huku akijua pamoja na kuwa na uwezo wa kuuondoa pasina kughafilika basi sala yake haitokubalika.

Kuna aina tatu za najis:-

NAJIS NYEPESI

(kwa mfano: mkojo wa mtoto wa kiume ambaye hajaanza kula, maji ya shahawa na mkojo mwepesi wa uchovu)

Huondolewa kwa kunyunyizia maji bila kuosha

NAJIS YA WASTANI

(kwa mfano: mkojo)

Huondolewa kwa kukoshwa kwa maji sehemu yenye najis hiyo

NAJIS NZITO

(kwa mfano: mate ya mbwa)

Huondolewa kwa kukiosha kile chombo mara saba mojawapo ikiwa kwa **kutumia mchanga**

VITU AMBAVYO NI NAJIS

Mkojo na kinyesi cha mwanadamu, mkojo na kinyesi cha mnyama aliyeharamishwa kuliwa, wanyama wawindaji wote isipokuwa wale wagumu kuwaepuka kama paka, damu inayotiririka kwa wingi baada ya kuchinja, damu inayotoka kwenye tupu mbili, maiti zote isipokuwa maiti tatu: maiti ya mwanadamu, maiti ya wadudu wasiokuwa na damu yenye kutiririka, maiti ya panzi na maiti ya mnyama anayeishi kwenye maji.

SHARTI LA SITA: KUSITIRI UCHI

Uchi umegawanyika sampuli tatu:-

UCHI MWEPESE

Huu ni uchi wa mtoto aliye na miaka saba hadi kumi.

Lazima asitiri tupu zake mbili

UCHI MZITO

Huu ni mwili mzima wa mwanamke aliyebaleghe na aliye huru (sio mtumwa); mwili wake mzima ni uchi isipokuwa uso.

Lazima asitiri uso wake pia akiwa mbele ya wanaume wasiokuwa maharimu wake.

UCHI WA WASTANI

Ni uchi wa waliobaki (ukitoa uchi mwepesi na wa mwanamke)

Lazima asitiri mwili wake kuanzia magotini hadi kwenye kitovu. Inapedekezwa pia kusitiri mabega.

SHARTI LA SABA: KUINGIA MUDA WA SALA

Sala haikubaliki kabla ya kuingia muda wake na baada ya kuondoka muda wake isipokuwa kujumuisha kwa udhuru wa kisheria. Mtu akikusudia kuchelewesha sala kutoka kwa muda wake bila ya udhuru wa kisheria basi sala hiyo haitokubaliwa.

SHARTI LA NANE: KUELEKEA QIBLAH

Kuelekea Qiblah ni jambo la lazima isipokuwa katika sala za Sunnah mtu akiwa safarini juu ya kipando chake au katika hali yetu ya kisasa; mtu akiwa kwenye ndege. Na pia hana dhambi kwa asiyekuwa na uwezo wa kuelekea Qiblah kutokana na uoga au maradhi.

SHARTI LA TISA: NIA

Nia pahala pake ni moyoni na kuitamka nia ni katika mambo ya uzushi. Akinuwia mtu kabla ya sala ya faradhi kwa muda basi sala yake ni sahihi.

TANBIHI MUHIMU

1. Haikubaliwi mtu kuacha sharti lolote kwa ujahili wala kusahau wala kusudi isipokuwa atakayesali na najis bila ya kujua basi huyo sala yake itakuwa sahihi.
2. Sharti linakuwa kabla ya ibada; nje ya ibada lakini lazima lipatikane hadi mwisho wa ibada husika.

SOMO LA SABA

NGUZO ZA SALA

Nguzo za Sala ni kumi na nne:-

- | | | |
|---|---------------------------------|---------------------------------------|
| 1. Kusimama kwa uwezo | 2. Takbiratul ihraam | 3. Kusoma Fatihah |
| 4. Kurukuu | 5. Kusimama wima baada ya rukuu | 6. Kusujudu kwa viungo saba |
| 7. Kuinuka kutoka sijda | 8. Kuketi baina ya sijda mbili | 9. Utulivu katika kila kitendo |
| 10. Utaratibu baina ya nguzo | 11. Tashahhud ya mwisho | 12. Kuketi kwaajili ya tashahhud hiyo |
| 13. Kumsalia Mtume kwenye tashahhud ya mwisho | 14. Salamu mbili | |

NGUZO YA KWANZA: KUSIMAMA KWA MWENYE UWEZO

SALA YA FARADHI

Kusimama ni nguzo katika sala ya faradhi na anasamehewa tu asiye kuwa na uwezo kabisa au uwezo wake akisimama utulivu wake unaondoka.

Akiwa na uwezo wa kusimama japo kidogo basi atasimama.

SALA YA SUNNAH

Inasihi sala yake akisali hali ya kuwa ameketi lakini atapata nusu ya thawabu ya yule aliyesali akiwa amesimama. Na akisali kwa kulala ubavuni basi atapata nusu ya thawabu ya aliyesali akiwa ameketi.

NGUZO YA PILI: TAKBIRATUL IHRAAM

Hii ni takbir ya kufunga sala. Na haikubaliki isipokuwa maneno haya: *Allahu akbar*

NGUZO YA TATU: KUISOMA SURATUL FATIAH

Ni lazima kuisoma suratul Fatihah, kisomo kamili kwa utaratibu wa mpangilio wa aya zake, katika kila rakaa ya sala; iwe sala za kupaza sauti au kisiri. Na anasamehewa akimuwahi imam kwenye rukuu.

NGUZO YA TISA: UTULIVU KATIKA KILA KITENDO

Utulivu unatimia kwa kusoma nyiradi zote za sala inavyotakiwa.

TANBIHI MUHIMU

Nguzo zinakuwa ndani ya ibada na haikubaliwi kuiacha nguzo kwa ujahili wala kusahau wala kusudi, na wala haijazwi kwa sijdatu sahwi (sijda ya kusahau) na inamlazimu mtu kuirudia ile au kuileta nguzo ile aloiacha. Lakini akikumbuka muda baada ya kumaliza sala yake basi hapo anasamehewa.

SOMO LA NANE

VITU VYA WAJIBU KATIKA SALA

Vitu vya wajibu katika sala ni vinane:-

1. Takbir zote kando na ya ihraam
2. Kusema: *samia Allahu liman hamida* (kwa imam na maamuma)
3. Kusema: *rabbanaa wa lakal hamd* (kwa wote wawili)
4. Kusema: *subhana rabbiyal athwiim* katika rukuu
5. Kusema: *subhana rabbiyal a^laa* katika sijda
6. Kusema: *Rabbi ighfir lii* baina ya sijda mbili
7. Tashahhud ya mwanzo
8. Kuketi kwaajili ya tashahhud ya mwanzo

TANBIHI MUHIMU

Ni wajibu kusema: *subhana rabbiyal athwiim* katika rukuu kutumia maneno haya kisha inapendekezwa azidishe nyiradi zingine zilizopokelewa.

Na pia ni wajibu kusema: *subhana rabbiyal a^laa* katika sijda kutumia maneno haya kisha inapendekezwa azidishe nyiradi zingine zilizopokelewa.

SOMO LA TISA

KUBAINISHA TASHAHHUD

Tashahhud ni kusema: *Attahiyyaatu lillahi wa sswalawaatu wa ttwayyibaatu. Assalaamu aleika ayyuha nnabiy wa rahmatullahi wa barakaatuh. Assalaamu aleinaa wa alaa ibaadillahi sswaalihin. Ash-hadu an laa ilaaha illa Allah wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh.*

Kisha anamsalia Mtume na kumuombea baraka kwa kusema: *Allahumma swalli alaa Muhammadin wa alaa aali Muhammadin kamaa swallaita alaa Ibrahima wa alaa aali Ibrahima innaka hamiidun majiid. Wa baarik alaa Muhammadin wa alaa aali Muhammadin kamaa baarakta alaa Ibrahima wa alaa aali Ibrahima innaka hamiidun majiid.*

Kisha anamuomba Allah amlinde kutokana na adhabu ya kaburini na adhabu ya motoni na kutokana na fitna za waliohai na waliokufa na kutokana na fitna ya masihi dajjal. Kisha anaomba dua yoyote atakayo na bora zaidi atumie zilizopokelewa kwa mfano: *“Allahumma ainniy alaa dhikrika wa shukrika wa husni ibaadatika. Allahumma inniy thwalamtu nafsiy dhulman kathiiran wa laa yaghfiru dhunuuba illa anta faghfir lii maghfiratan min indika wa-r-hamniy, innaka antal ghafuuru rahiim.”* (Ewe Mol wangu hakika mimi niko katika utajo Wako na shukrani Zako na bora ya ibada Zako. Ewe Mola wangu, hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma nyingi na najua kuwa hakuna anayesamehe madhambi isipokuwa Wewe. Naomba unisamehe msamaha kutoka Kwako ambao haubakishi dhambi lolote na unirehemu kwani Wewe ndiye mwenye kurehemu.)

Ama katika tashahhud ya mwanzo katika swala ya Dhuhur, Asr, Maghrib na Isha; atasimama baada ya kutoa shahada katika tashahhud na akimsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, itakuwa bora.

SOMO LA KUMI

SUNNAH ZA SALA

Miongoni mwa Sunnah za sala ni:-

1. Dua ya ufunguzi wa sala
2. Kuuwekelea mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto kwenye kifua wakati wa kusimama, kabla ya rukuu na baada ya rukuu.
3. Kunyanyua mikono miwili, huku umetawanya vidole, hadi urefu wa mabega au masikio wakati wa takbiratul ihram, kuenda rukuu, kutoka rukuu na kutoka tashahhud ya mwanzo kwa ajili ya kusimama rakaa ya tatu.
4. Kuzidisha nyiradi zaidi ya mara moja katika rukuu na katika sijda.
5. Kuleta nyiradi za ziada baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu.
6. Kusawazisha baina ya kichwa na mgongo katika rukuu
7. Kutenganisha baina ya viwiko na mbavu na baina ya tumbo na mapaja katika hali ya kusujudu.
8. Kuweka mikono juu kutoka kwa ardhi katika hali ya kusujudu. (kiwiko kisiguse ardhi)
9. Kuketi juu ya mguu wa kushoto uliotandazwa na kuusimamisha mguu wa kulia katika kikao cha tashahhud ya mwanzo.
10. Kuketi kikao cha *tawarruk* katika kikao chao tashahhud ya mwisho: kuketi kitako huku mguu wa kulia umesimama na kuupitiza mguu wa kushoto chini ya mguu wa kulia.
11. Kuashiria katika sala wakati wa tashahhud zote mbili kutumia kidole cha shahada kuanzia mwanzo wa tashahhud hadi mwisho na kukitikisa wakati wa dua.
12. Kumsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na kumtakia baraka kwenye tashahhud ya mwanzo.
13. Dua kwenye tashahhud ya mwisho.
14. Kupaza sauti kwa kisomo kwenye sala za AlFajr, Ijumaa, idi mbili, sala ya mvua na kwenye rakaa mbili za mwanzo za sala ya Maghrib na Isha.
15. Kuficha sauti kwa kisomo kwenye sala za Dhuhur, Asr, rakaa ya tatu ya sala ya Maghrib na rakaa mbili za mwisho kwenye sala ya Isha.
16. Kusoma surah nyingine baada ya suratul Fatihah.

DUA YA UFUNGUZI WA SALA

Inakuwa dua hii ya ufunguzi baada ya takbiratul ihraam kama ilivyopokelewa kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kwa maneno haya: *“Allahumma baaid bainiy wa baina khatwaayaa kamaa baa^adta bainal mashriq wal maghrib. Allahumma naqqiniy minal khatwaayaa kamaa yunaqqa th-thaubul ab-yadhu mina ddanas. Allahumma ighsilniy min khatwaayaa bilmaai wa th-thalji wal barad.”*

Au kauli hii: *“Subhaanaka Allahumma wa bihamdika, wa tabaaraka ismuka wa taala jadduka, wa laa ilaaha ghairuka.”*

SOMO LA KUMI NA MOJA

MAMBO YANAYOVUNJA SALA

Mambo yanayovunja sala ni manane:-

1. Kucheka
2. Kula
3. Kunywa
4. Kufichua uchi
5. Kuacha kuelekea Qiblah kipande kikubwa cha mwili
6. Harakati nyingi mutawalii
7. Kutenguka kwa twahara (hali ya usafi)
8. Kuzungumza kwa kusudi ndani ya sala pamoja na kuwa mtu anafahamu uharamu wake. (ama aliyesahau au hajui mafundisho hayo basi sala yake haijahiribika).

JAMBO LA NANE: KUZUNGUMZA KUSUDI PAMOJA NA KUJITAMBUA

Hairuhusiwi kuzungumza katika sala maneno yasiyohusiana na sala. Anaruhusiwa tu mtu kumkumbusha imam wakati imam kakosea au kasahau jambo katika sala.

HARAKATI KATIKA SALA

Harakati ya lazima ambayo kukubalika kwa sala kunaitegemea kama kuondoa najis

Harakati ambayo inapendekezwa kwa sababu inaleta ukamilifu wa ziada katika sala kama kuziba pengo katika safu.

Harakati ambayo imeruhusiwa kama kujikuna kwenye ndevu kwa haja.

Harakati ambazo zinachukiza pasina dharura kwa mfano kugeuza macho kando

Harakati ambazo zimeharamishwa nazo ni harakati nyingi mfululizo pasina dharura kwa mfano: *kula*

TANBIHI MUHIMU

TOFAUTI BAINA YA SHARTI, NGUZO, WAJIBU NA SUNNAH KATIKA SALA

SHARTI	NGUZO	WAJIBU	SUNNAH
Inapatikana nje ya sala	Zinapatikana ndani ya sala		
Inaendelea hadi mwisho wa sala	Zinapatikana kwenye vipengele maalum katika sala		
Haisameheki kuacha kwa ujahili wala kusahau wala kusudi.		Inasameheka kuacha kwa ujahili na kusahau wala sio kwa kusudi	Inasameheka kuacha kwa ujahili, kusahau na kusudi.
Haina sijdatu sahwi (sijda ya kusahau)	Hailipwi kwa sijdatu sahwi	Hulipwa kwa sijdatu sahwi	/

SIJDATU SAHWI (SIJDA YA KUSAHAU KITU KATIKA SALA)

Hii sijda huletwa kwa sababu moja miongoni mwa sababu hizi tatu:-

KUZIDISHA

Kwa mfano mtu kuzidisha rukuu au sijda au kikao kwenye sala.

KUPUNGUZA

Kwa mfano mtu kupunguza jambo la wajibu katika mambo ya wajibu katika sala. Akaliacha kutoka sehemu yake.

SHAKA

Kama kutatasika mtu hajui amesali rakaatatu ama nne.

Na shaka imegawanyika aina mbili:-

SHAKA BAADA YA KUMALIZA SALA

Aina hii ya shaka haizingatiwi kabisa isipokuwa awe na yakini.

SHAKA NDANI YA SALA

- Ikiwa ni shaka nyingi basi asiizingatie
- Ikiwa ni shaka chache, ajenge kwa lile alilo na yakini nalo
- Ikiwa shaka na yakini zimetoshana, basi achague ile ndogo (*kwa mfano hajui amesali rakaatatu au nne wala hana jambo la kurajihisha moja yao basi inafaa aseme amesali rakaatatu maana ndio yenye uhakika*)

MAELEKEZO MUHIMU

1. Akisahau mtu kusujudu sijda ya sahwibasi hana dhambi na sala yake ni sahihi
2. Mtu akiacha nguzo ya sala, hiyo sala haikubaliwi na lazima ailete nguzo ile na kisha asujudu sijda ya sahwimwisho wa sala yake.
3. Akiacha mtu jambo ambalo ni wajibu katika sala na ashaondoka sehemu ya wajibu ile basi inamtosheleza kusujudu tu sijda ya sahwimwisho wa sala yake.

MAFUNDISHO YA SALA KWA UFUPI

- Ajitwahirishe Muislamu nyumbani kwake na avalie mavazi nzuri.
- Aelekee msikitini – kwa miguu au kipando – kwa utulivu na taratibu wala asikimbie wala kutizama sana mambo ya dunia wala asinyanyue sauti yake.



- Akifika msikitini, avue viatu vyake na aviweke sehemu maalum ya kuweka viatu na aweke pia dunia sehemu hiyo ya viatu; asianze biashara ndani ya msikiti wala asitangaze msikitini kitu kilichopotea.
- Na autangulize mguu wake wa kulia katika kuingia msikitini na aseme dua hii: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillaah. Allahumma iftah lii abwaaba rahmatika.* Na wakati wa kutoka atangulize mguu wa kushoto na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillaah. Allahumma inniy as-aluka min fadhlika.*
- Wanaume waketi kwenye safu za mbele na wanawake bora ya safu zao ni safu zile za mwisho.
- Ikiwa sala tayari imeanza, basi alete takbiratul ihraam, afunge sala na amfuate imam atakapompata: Anahesabu rakaa kamili akimpata imam amesimama au katika rukuu. Na imam akitoa salamu basi asimame aliye yaliyompita.
- Lakini ikiwa ameingia msikitini na sala haijaanza, basi atasali sala za Sunnah au Sunnah ya kuingia msikitini.
- Wala haifai kuleta jambo la kushawishi kuashiria sala ianze. Kwa mfano kila wakati kutizama saa au kubuni kikohozi kama ishara.
- Inapendekezwa aweke sutra/kizuizi mbele yake akiwa anasali pekee lakini kama anasali nyuma ya imam basi imam ndiye sutra ya walioko nyuma yake.




- Na aweke miguu yake kama kiasi kilicho baina ya mabega yake bila kuzidisha wala kupunguza.



- Baada ya kutimiza masharti yote ya sala, aseme **Allahu akbar** huku akiinua mikono yake urefu wa wa mabega au masikio akiwa vidole vimeshikana na aelekeze sehemu ya ndani ya viganja Qiblah.



- Kisha auweke mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto kwa kubana au kutelekeza.



- Na aelekeze macho yake pahala pa kusujudu wala asitizame huku na kule.



- Kisha inapendekezwa asome dua ya ufunguzi katika rakaa ya mwanzo pekee na bora akitumia nyiradi tofauti tofauti za ufunguzi katika sala zake.
- Kisha ajilinde kwa Allah kwa kusema: **Audhu billahi mina sh-shaitwani rrajiim**
- Kisha aseme: **Bismillahi Rrahmani Rrahiim**
- Kisha aisome suratul Fatihah kamili kwa utaratibu na nidhamu ipasavyo.
- Kisha aisome surah nyingine baada ya Fatihah kadri ya uwezo.
- Kisha ainue mikono kama alivyoinua kwenye takbiratul ihraam na aseme: **Allahu akbar** kisha aende rukuu.
- Aishike magoti yake kwa viganja wala asikunje viwiko vyake na aunyooshe mgongo wake ausawazishe na kichwa.
- Aseme akiwa kwenye rukuu: **Subhana rabbiyal athwiim** mara moja au zaidi.




- Kisha anyanyuke kutoka rukuu huku akisema: *Samia Allahu liman hamida*. Ainuke pamoja na kunyanyua mikono yake urefu wa mabega au masikio.
- Akiwa amenyooka wima kabisa aseme: *Rabbanaa wa lakal hamd*.
- Kisha alete Takbir bila kunyanyua mikono na asujudu kwa viungo saba: *paji la uso, pua, viganja viwili, magoti mawili na miguu miwili*.
- Aweke mbali baina ya viwiko na tumbo na baina ya tumbo na mapaja.



- Na aseme akiwa amesujudu: *Subhana rabbiyal a'laa* mara moja au zaidi.
- Kisha aketi kama kikao cha tashahhud kama tulivyoelezea.



- Kisha asujudu tena kama sijda ya kwanza
- Kisha alete Takbir na asimame kwaajili ya kutekeleza rakaa ya pili bila ya kuleta dua ya ufunguzi.
- Akikamilisha sijda ya pili katika rakaa ya pili ataketi kikao cha tashahhud na kuleta tashahhud huku amefanya duara kidole chake cha gumba.
- Kama ni sala ya rakaa mbili basi atamsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na amuombe Allah amlinde kutokana na shari zote.
- Kisha atatoa salamu mbili; moja pande ya kulia na nyingine pande ya kushoto kwa kugeuza kichwa pande zote mbili wala sio kwa kugeuza mabega.



- Na ikiwa sala ni ya rakaa tatu au nne, basi baada ya tashahhud ya kwanza, atasimama ili kukamilisha rakaa zilizobaki.
- Ikiwa ni sala ya faradhi basi inapendekewa kuleta nyiradi za baada ya sala.

TANBIHI MUHIMU

- Kama ilivyotangulia kwenye masharti ya sala katika kusitiri uchi. Basi lazima ajisitiri isifichuke uchi isije haribika sala yake.



- Akisali mtu na imam, basi asimame upande wa kulia mwa imam na alilinganishe bega lake na la imam.



JEDWALI LA MUKHTASAR WA SALA

SALA	HUKUMU	MUDA WAKE	RAKAA	SIFA
Jumuah	Faradhi	Wakati wa sala ya Dhuhur	Rakaa mbili	Inasaliwa kwa kupaza sauti na kwa jamaa ya watu kuanzia watatu
Kusuuf	Faradhi kifaya (inatoshleza baadhi ya watu wakiisali)	Ikitokea kushikana jua na mwezi	Rakaa mbili	Inasaliwa kwa kupaza sauti na ina rukuu mbili kwa kila rakaa moja
Witri	Sunnah iliyosisitizwa	Baada ya sala ya isha hadi AlFajr	Kuanzia rakaa moja hadi kumi na moja.	Ikiwa rakaa moja au zaidi tashahhud itakua katika rakaa ya mwisho.
Sunnah ya Fajr	Sunnah iliyosisitizwa	Kabla ya sala ya Fajr	Rakaa mbili	Inasomwa rakaa ya kwanza baada ya Fatihah suratul Kaafiruun na rakaa ya pili Ikhlalas.
Sunnah ya Dhuhur	Sunnah	Rakaa nne kabla ya Dhuhur na rakaa mbili baada yake	4/2	Rakaa mbili kisha salamu kisha rakaa mbili tena
Sunnah ya Maghrib	Sunnah	Baada ya sala ya Maghrib	Rakaa mbili	Inasomwa rakaa ya kwanza baada ya Fatihah suratul Kaafiruun na rakaa ya pili Ikhlalas.
Sunnah ya Isha	Sunnah	Baada ya sala ya Isha	Rakaa mbili	
Taraweh	Sunnah	Baada ya sala ya Isha hadi Fajr	Kuanzia rakaa mbili hadi rakaa kumi	
Tahiyatul Masjid	Wajib	Kuingia msikitini kabla ya kuketi	Rakaa mbili	
Dhuha	Sunnah	Kuchomoza jua hadi kabla ya kupinda	Kuanzia rakaa mbili hadi nane	
Istikhara	Sunnah	Muda wowote	Rakaa mbili	Anaomba dua ya istikharra kabla ya salamu
Istisqaa	Sunnah kwa haja	Baada ya kuchomoza jua wakati wa kiangazi	Rakaa mbili	Analeta Takbir saba baaada ya takbiratul ihraam na tano akiamka rakaa ya pili
Eid	Sunnah	Baada ya kuchomoza jua kadri ya urefu wa mkuki	Rakaa mbili na khutbah mbili	Analeta Takbir saba baada ya takbiratul ihraam na tano akiamka rakaa ya pili

NYAKATI ZILIZOKATAZWA KUSALI

1. Kuanzia baada ya AlFajr hadi kuchomoza jua
2. Kuanzia Asr hadi Maghrib
3. Kusimama jua utosini hadi kupinda

MASUALI KUHUSU SALA

1. Masharti ya Sala ni ngapi?
 - ☐ 9
 - ☐ 11
 - ☐ 8
2. Upambanuzi ni nguzo au sharti ya Sala?
3. Je. Ni lazima kusafisha mwili, nguo na pahala pa Sala?
4. Najis ya nguruwe ni aina gani ya najis?
 - ☐ Nyepesi
 - ☐ Ya wastani
5. Je. Manii ni najis?
6. Tofauti baina ya kuosha na kunyunyizia. **Kuosha** ni **Kunyunyizia** ni
7. Maiti zote ni najis isipokuwa
8. Mdudu asiye kuwa na damu yenye kutiririka maiti yake najis (ni /sio)
9. Je. Damu inayobaki mishipani ni najis?
10. Nguzo za Sala ni ngapi?
11. Je. Mtu akiacha nguzo kwa kusahau, ataleta sijdatu sahwi pekee?
12. Mambo ya wajibu katika Sala ni ngapi?
 - ☐ 8
 - ☐ 14
 - ☐ 9
13. Ni sheria kuuweka mkono wa kushoto juu ya mkono wa kulia kawaida?
14. Mambo yanayovunja sala ni mambo
15. Kikao cha Tawarruk kinakua katika tashahhud ya (mwanzo / mwisho)
16. Uradi baina ya sijda mbili ni:
17. Kiwiko kugusa ardhi katika sijda ni
 - ☐ Haramu
 - ☐ Sunnah
 - ☐ Inachukiza
18. Sababu za sijdatu sahwi ni ngapi?
 - ☐ 2
 - ☐ 3
 - ☐ 4
19. je shaka baada ya sala inaathiri?

20. Bainisha hukumu ya vitu vifuatavyo:-

JAMBO	HUKUMU YAKE
Sala ya mtu anayemtusi Allah	
Sala ya mlevi	
Sala ya mtu mwenye kifafa	
Sala ya mtoto	
Sala bila Wudhuu	
Sala kwa nguo yenye najis	
Mkojo wa ng'ombe	
Mkojo wa kunguru	
Sala hali ya kuwa mapaja yako wazi	
Sala kabla ya muda kwa kusahau	
Sala ndani ya ndege	
Sala kwa kuketi	
Kusahau kuisoma Fatihah katika sala	
Kumpata imam katika rukuu	
Kukimbilia sala	
Shaka nyingi kwenye sala	
Kushuku Wudhuu baada ya sala	
Kuzidisha rukuu kwa kusahau	
Kuiacha takbiratul ihraam	
Kuiacha tashahhud ya mwanzo	
Kuiacha tashahhud ya mwisho	
Kushuku amesali rakaa tatu au nne	
Shaka baada ya sala	
Shaka ndani ya sala	
Kusahau kuileta sijdatu sahwi	
Kusali uchi ukionekana bila kujua	
Kujitwahirisha nyumbani	
Biashara msikitini	
Kubadilisha sarafu msikitini	
Kuzungumza katika sala kwa kusahau	
Kumdiriki imam kwenye tashahhud	
Kujisitiri uchi katika sala	
Kutembeza macho katika sala	
Kusali kwa kasi	
Kumsalia Mtume	
Kuzidisha jambo katika sala	
Harakati nyingi katika sala	
Kuisahau Fatihah	
Sala ya Jumuah	

21. Elezea tofauti baina ya nguzo, sharti, wajibu na Sunnah katika sala.

SOMO LA KUMI NA MBILI

MASHARTI YA WUDHUU

Masharti ya Wudhuu ni kumi:-

1. Uislamu
2. Akili timamu
3. Upambanuzi
4. Nia
5. Asinuwie kuvunja Wudhuu hadi mwisho wa kutawadha
6. Kupatikana jambo linalowajibisha Wudhuu
7. Kukidhi haja
8. Maji yawe safi
9. Kuondoa kinachozuia maji kufikia ngozi
10. Kuingia muda wa sala kwa asiyekuwa msafi

SUNNAH ZA KIMAUMBILE

Katika mambo ya kimaumbile ambayo lazima kila Muislamu ayazingatie ni:-

(LA KWANZA): Kutahiriwa kwa watoto wa kiume.

(LA PILI HADI LA TANO): kupunguza masharubu, kukata kucha, kung'oa nywele za kwapa na kunyoa nywele za sehemu za siri. Anasema Anas, Allah awe radhi naye, *“Imeekwa kuwa kupunguza masharubu, kukata kucha, kung'oa nywele za kwapa na kunyoa nywele za sehemu za siri isipite siku arbaini.”* Basi haifai kusubiri hadi siku 40 ziishe.

(LA SITA): kufuga ndevu: kuzifuga ni wajibu na kuzinyoa ni katika dhambi kubwa.

(LA SABA): mswaki: inasisitizwa kupiga mswaki kila mara mtu anapotawadha, wakati wa sala, kuingia nyumbani, kusoma Kur'ani, kulala na inapobadilika harufu kinywani.

SOMO LA KUMI NA TATU

FARADHI ZA WUDHUU

Faradhi za Wudhuu ni sita:-

1. Kuosha uso pamoja na kusukutua na kuosha pua
 2. Kuosha mikono miwili hadi kwenye viwiko
 3. Kupangusa kichwa kwa mikono nyevunyevu pamoja na masikio
 4. Kuosha miguu miwili hadi kwenye vifundo viwili vya miguu.
 5. Taratibu katika kuosha viungo
 6. Upesi katika kuosha viungo (aoshe kiungo kabla cha kabla yake kukauka)
- Inapendekezwa kuosha uso, mikono miwili na miguu miwili mara tatu na vilevile katika kuosha pua na kusukutua. Lakini faradhi ni kuosha viungo vyote mara moja. Na haipendekezwi kupangusa kichwa zaidi ya mara moja.

SOMO LA KUMI NA NNE

MAMBO YANAYOTENGUA WUDHUU

Mambo yanayovunja Wudhuu ni sita:-

1. Kinachotoka kwenye tupu mbili
2. Na kinachotoka mwilini katika vitu najis
3. Kupoteza fahamu kwa njia ya usingizi
4. Kugusa tupu mbili kwa kiganja bila ya kizuizi
5. Kula nyama ya ngamia
6. Kuritadi (kutoka katika Uislamu)

TANBIHI MUHIMU

Ama kumuosha maiti, kauli sahihi ni kuwa haitengui Wudhuu. Na hii ndio kauli ya wanazuoni wengi; kwa sababu hakuna dalili ya kudhibitisha hilo. Lakini lau mkono wa muosha maiti itaugusa utupu wa maiti bila kizuizi basi itamlazimu kutawadha. Na ni wajibu kwa muosha maiti kutogusa utupu wa maiti isipokuwa kwa kizuizi.

Na vilevile kumgusa mwanamke hakutengui Wudhuu kabisa; ima amemgusa kwa matamano au bila matamano maadamu hajatokwa na manii. Na hii ndio sahihi katika kauli mbili za wanazuoni kwa sababu Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alikuwa akibusu wakeze kisha anaenda kusali pasina kutawadha.

Na makusudio ya aya namba 6 katika suratul Maidah inayosema *au laamastumu nnisaa (au mmewagusa wanawake)* makusudio ya kugusa kwenye ayah hii ni kuingiliana kwende tendo la ndoa. Hii ndio kauli ya Ibn Abbas na kikundi katika wema waliotangulia, Allah awe radhi nao.

MAFUNDISHO YA JINSI YA KUTAWADHA KWA UFUPI

- Akishanuwia Wudhuu basi aseme: *Bismillahi*
- Aoshe viganja viwili kabla ya kuvitumbukiza kwenye chombo cha maji
- Achukue maji kwa mkono wa kulia kuingiza mdomoni, asukutue na aoshe pua lake huku akitoa uchafu puani kwa kutumia mkono wa kushoto.
- Aoshe uso wake mara tatu kuanzia kidevu hadi mwanzo wa nywele za kichwani na kuanzia sikio hadi sikio la pili.
- Aoshe mikono miwili hadi kwenye viwiko mara tatu akianza na mkono wa kulia kisha kushoto.
- Kisha apanguse kichwa kuanzia mwanzo wa hadi mwisho
- Kisha atumbukize kidole cha shahada kwenye sikio aipanguse
- Kisha aoshe miguu yake miwili pamoja na vifundo mara tatu.





Kisha aseme anapomaliza Wudhuu wake: *ash-hadu an laa ilaaha illa Allahu wahdahu laa shariika lahu, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh. Allahumma ij-alniy mina ttawwaabiina waj-alniy minal mutatwahiriiin.*

(Nashuhudia kuwa hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake. Ewe Mola wangu, nijaalie niwe miongoni mwa wanaotubu na nijaalie niwe miongoni mwa waliotwahirika.)

HUKUMU YA KUZIDISHA KIWANGO KILICHOPOKELEWA

Haifai kuzidisha kiwango kilichopokelewa katika Wudhuu. Kwa mfano kuzidisha zaidi ya mara tatu katika kuosha viungo au kuosha mkono hadi kwenye kwapa au kupangusa shingo.

MAMBO YANAYOAMBATANA NA NGUZO ZA UISLAMU

KWANZA: TWAHARA KUTAYAMAM

Hii ni aina ya twahara mbadala ya maji kwa yule asiyekuwa na uwezo wa kutumia maji au amekosa maji au anahofia kuyatumia kwa sababu ya madhara ya kiafya. Inakuwa kwa kutumia mchanga.

SIFA YA KUTAYAMAM

Anuwie kisha aseme *Bismillahi* kisha apige ardhini kwa viganja viwili mara moja na apanguse uso wake na sehemu ya nje ya viganja vyake.



Wala haifai kunawa mikono kwa mchanga.



SIFA YA WAJIB YA GHUSL (KUOGA)

Anuwie kuoga na kuondoa hadith kubwa kisha aseme *Bismillahi* kisha aoge mwili mzima huku akihakikisha kuwa maji yameingia kila sehemu ya mwili; ikiwemo ndani ya nywele na asukutue pamoja na kuosha pua.

SIFA YA SUNNAH KATIKA KUOGA

Aoshe tupu mbili kisha viganja viwili kisha atawadhe kama anavyotawadha kwaajili ya sala kisha aingize maji kwenye nywele zitote kisha aoshe mwili wake upande wa kulia kisha kushoto kisha aoshe miguu.

MAMBO YANAYOWAJIBISHA KUOGA

1. JANABA: na inakuwa kwa kutokwa kwa manii kwa kuingiliana au mengine.
2. Kutokwa damu ya hedhi na damu ya uzazi
3. Kifo (isipokuwa aliyekufa katika jihad)
4. Mtu anaposilimu

MASHARTI YA KUPANGUSA SOKSI (KHUFEIN NA JAURABU)

Azivalie baada ya kutawadha Wudhuu kamili; yaani: kaosha miguu vyema katika Wudhuu wake.

Ziwe zimeundwa kwa vitu twaahir (vitu visivyokuwa najis)

Ziwe zimesitiri miguu kwa kiwango kikubwa

Iwe kupanguswa kwao ni katika hadath ndogo sio hadath kubwa.

Iwe muda wa kupangusa ni ule uliowekwa na sheria. Nayo ni: masaa ishirini na nne (24) kwa asiyekuwa msafiri kuanzia alipovunja Wudhuu akiwa nazo na masaa sabini na mbili (72) kwa msafiri kuanzia muda aliovunja Wudhuu akiwa amezivalia.

JINSI YA KUPANGUSA KWENYE SOKSI WAKATI WA KUTAWADHA

Aupitize mkono kutumia viganja kuanzia vidole vya mguu hadi karibu na muundi wa mguu; mkono wa kulia kwa mguu wa kulia na wa kushoto kwa mguu wa kushoto. Wala asipanguse sehemu ya chini ya miguu.

MASUALA YANAYOHUSIANA NA UPANGUSAJI WAKE

1. Ukiisha muda wa kupangusa au akazivua , basi Wudhuu wake unabaki wala hautenguki.
2. Inaruhusiwa kuzipangusa soksi zilizochanika au nyepesi.

ADABU ZA KUKIDHI HAJA

Inapendekezwa:-

- Anapoingia msalani, autangulize mguu wake wa kushoto na aseme: *Bismillahi. Allahumma inniy audhu bika minal khubthi wal khabaaith.*
- Na akitoka msalani autangulize mguu wa kulia na aseme: *Ghufraanaka.*

Ni **wajibu** ajisitiri wakati wa kukidhi haja na aende mbali na macho ya watu ikiwa katika jangwa

Na **sio ruhusa**:-

- Kukidhi haja barabarani au sehemu wanapoketi watu au chini ya kivuli cha mti wa matunda au sehemu ya kuwaudhi watu au kwenye maji yaliosimama.
- Kuelekea Qiblah au kuupa mgongo katika hali ya kukidhi haja.
- Kugusa utupu wake kwa mkono wa kulia.
- Kulitaja jina la Allah msalani.

Akishakidhi haja, achambe kwa maji safi au kwa kutumia mawe au mbadala. Na masharti ya kutumia mawe na mbadala ni:-

- Yawe mawe matatu au jiwe lenye pande tatu ili ajipanguse mara tatu.
- Yawe mawe/mbadala safi (yani karatasi au jiwe kavu)
- Isikuwe kujipangusa kwa kitu najis au chakula au mifupa au kinyesi.

Na ni ruhusa kukojoa hali ya kuwa amesimama kwa sharti; ule mkojo usimtonokee/rukie mwilini au kwenye nguo na asitiri uchi wake. Kwa dalili kuwa: *Mtume, rehma na amani ziwe juu yake, alifika kwenye makidhi ya kabila moja akakidhi haja ndogo hali ya kuwa amesimama.*

1. Masharti ya Wudhuu ni ngapi?

- ☐ 9
- ☐ 10
- ☐ 8

2. Faradhi za Wudhuu ni

- ☐ Viungo vinne
- ☐ Viungo vinne pamoja na taratibu na upesi katika kuosha viungo

3. Mambo yanayotengua Wudhuu ni ngapi?

- ☐ 6
- ☐ 5
- ☐ 8

4. Bainisha yafuatayo:-

- ☐ Nyama ya ngamia:
- ☐ Nyama ya kunguru:
- ☐ Mngurumo tumboni:
- ☐ Kujamba:
- ☐ Kusinzia:
- ☐ Kuosha maiti:
- ☐ Kungusa mwanamke:

5. Taja sifa ya Wudhuu:

.....

.....

.....

6. Taja sifa za ghusl:

.....

.....

.....

7. Taja hukumu ya kila lifuatalo:-

SUALA	HUKUMU
Kuitamka nia	
Kunuwia kwa Wudhuu wake sala moja	
Kutawadha kwa lengo la kusoma Kur'ani	
Kuvunja nia katikati ya Wudhuu	
Kuvunja nia baada ya Wudhuu	
Kutawadha huku anakula karoti	
Kutawadha kwa maji ya wizi	
Kutawadha kabla ya kukidhi haja	
Kupangusa sikio kwa maji mapya	
Kupangusa kichwa mara tatu	
Kuosha viungo mara tatu katika Wudhuu	
Kuosha viganja viwili katika Wudhuu	
Kulowesha ndevu	
Kujisugua katika Wudhuu	
Kuosha viungo vipasavyo kupanguswa	
Kuosha kichwa	
Kutumbukiza viganja kwenye chombo	
Kuanza kwa upande wa kulia katika Wudhuu	
Kuosha viungo zaidi ya mara tatu	
Kuosha miundi ya miguu	
Kusali baada ya kuogelea	
Kusali baada ya kuoga na bila kutawadha	

PILI: ZAKAH
AINA ZA ZAKAH:-

ZAKAH YA MALI

Hii ni nguzo ya tatu katika nguzo za Uislamu. Na ni wajibu kwa kila Muislamu aliye huru anayemiliki mali iliyofikia kiwango cha kutolewa. Na hakuna kulazimika zakah hadi itakapopitiwa na mwaka mzima isipokuwa mali inayotoka ardhini (mazao ya ukulima)

Na mali inayotolewa zakah ni ya aina nne:-

ZAKAH YA MWILI

Hii ni zakatul fitri inayotolewa baada ya kuumaliza mfungo wa Ramadhani. Ni wajibu kutolewa kwa kila Muislamu; mkubwa kwa mdogo, kike kwa kiume, mtumwa na aliye huru.

HELA

Hii ni dhahabu, fedha na yanayotumika kama dhahabu na fedha katika miamala za kibiashara.

Kiwango cha kutoa zakah cha hela:-

Dhahabu: gramu 85

Fedha: gramu 595

MIFUGO

Hawa ni mifugo ambao huenda malishoni. Mifugo hawa ni: ngamia, mbuzi, kondoo na ng'ombe.

MAZAO YA ARDHI

Haya ni mazao yanayotoka ardhini katika mimea kwa mfano: mbegu na matunda.

BIDHAA ZA BIASHARA

Hiki ni kila kilichoandaliwa kwa makusudio ya kibiashara

WANAOPASWA KUPEWA ZAKAH

1. **FAKIRI:** huyu ni mtu ambaye hapati mahitaji yake ya dharura au anapata kisichomtosha.
2. **MASKINI:** huyu ni mwenye kupata mahitaji yake ila sio kiukamilifu.
3. **WAKUSANYA ZAKAH:** hawa ni wale waliotwikwa majukumu ya kukusanya, kuhifadhi na kuigawanya zakah kwa wanaostahiki. Na hawa sio lazima wawe maskini au fukara. Bali wanapewa hata kama ni matajiri.
4. **WALAINISHWA NYOYO:** hawa ni wale unaotarajiwa kusilimu kwao, kuzuia shari zao au kuhifadhi nguvu za imani yao.
5. **UTUMWA:-** hawa ni
 - Mtumwa Muislamu anayenunua uhuru wake kutoka kwa mola wake.
 - Kumwacha huru mtumwa Muislamu.
 - Mateka MuislamuNa wala haingii katika hawa, mtumwa alieachwa huru na mola wake kama zakah yake. Hili halifai.
6. **WANAODAIWA:** hawa ni
 - Aliyebeba gharama kwa lengo la kusuluhisha baina ya wagomvi.
 - Aliyebeba gharama kwa lengo la kukidhi mahitaji yake.Na wala haifai kumsamehe deni mdaiwa kwa lengo la kukusudiwa zakah.
7. **KWA NJIA YA ALLAH:** hii inakusudiwa chochote kinachofanywa kwa njia ya Allah ikiwemo kuwaandaa wapiganaji wa jihad na wanayoyahitaji kama silaha na mengine.
8. **MSAFIRI:** aliyekatikiwa na safari kwa kuishiwa nafaka yake ya safari. Huyu anapewa kitakachomwezesha kuikamilisha safari yake.
Inaruhusiwa kukipa kikundi kimoja katika hawa zakah, wala hairuhusiwi katika zakah kumpa tajiri wala mchumaji wala ahli zake Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, wala kizazi cha Bani Hashim na wajakazi wao wala kuwapa wale inayomlazimu lishe yao wala kafiri.
Inaruhusiwa katika **sadaka ya kujitolea**, kumpa yeyeto yule.

MAANA YA BAADHI YA MISAMIATI ZINAYOTUMIKA KATIKA ZAKAH

- **BINTUL MAKHAADH:** ni ngamia aliyetimiza mwaka mmoja
- **BINTU LABUUN:** ni ngamia aliyetimiza miaka miwili.
- **AL-HIQQAH:** ni ngamia aliyetimiza miaka mitatu.
- **AL-JADH[^]AH:** ni ngamia aliyetimiza miaka minne.
- **AT-TABI[^]AH KATIKA NG'OMBE:** huyu ni ng'ombe mwenye mwaka mmoja.
- **AL-MUSINNAH:** ng'ombe mwenye miaka miwili.

VIWANGO VYA KUTOA ZAKAH

AINA YA MALI	SHARTI LAKE	KIWANGO CHA MALI	KIWANGO KINACHOTOLEWA
MIFUGO WENYE LISHE HURU	Lazima ipitiwe na mwaka	Angalia jedwali ijayo	Angalia jedwali ijayo
MAZAO YA ARDHINI	Sio lazima ipitiwe na mwaka	Kilogramu 612	- Ushuru yake kama mavuno yalikuwa kupitia maji ya mvua - Nusu ya ushuru kama mavuno yalikuwa kupitia kunyunyiziwa kwa mikono. - Robo tatu ya ushuru kama mavuno yalikuwa kwa njia zote mbili.
HELA	Lazima ipitiwe na mwaka	Dhahabu: gramu 85 Fedha: gramu 595	Asilimia mbili na nusu (2.5%)
BIDHAA ZA BIASHARA	Lazima ipitiwe na mwaka	Italinganishwa na bei nafuu baina ya kiwango cha dhahabu gramu 85 au fedha gramu 595.	Asilimia mbili na nusu (2.5%)

VIWANGO VYA ZAKAH YA MIFUGO

MBUZI NA KONDOO		NGAMIA		NG'OMBE NA NYATI	
KIWANGO	ZAKAH	KIWANGO	ZAKAH	KIWANGO	ZAKAH
Kuanzia 40 hadi 120	Mbuzi mmoja	Kuanzia 5 hadi 9	Mbuzi mmoja	Kuanzia 30 hadi 39	Tabii^ah
Kuanzia 121 hadi 200	Mbuzi wawili	Kuanzia 10 hadi 14	Mbuzi wawili	Kuanzia 40 hadi 59	Musinnah
Kuanzia 201 hadi 300	Mbuzi watatu	Kuanzia 15 hadi 19	Mbuzi watatu	Kuanzia 60 hadi 69	Tabii^ah wawili
Zaidi ya 300	Mbuzi mmoja kwa kila mbuzi 100.	Kuanzia 20 hadi 24	Mbuzi wanne	Kuanzia 70 na zaidi	Katika kila 30 atatoa tabii^ah mmoja au katika kila 40 atatoa musinnah mmoja.
Haikubaliwi mbuzi kengeza, chongo, kipofu au mwenye aibu kubwa mwilini.		Kuanzia 25 hadi 35	Bint makhaadh		
Haikubaliwi walio chini ya kiwango cha miaka – wadogo zaidi		Kuanzia 36 hadi 45	Bint labuun		
		Kuanzia 46 hadi 60	Hiqqah		
		Kuanzia 61 hadi 75	Judh^ah		
		Kuanzia 76 hadi 90	Bint labuun wawili		
		Kuanzia 91 hadi 120	Hiqqah wawili		
		Kuanzia 121 hadi 129	Bint labuun watatu		
		Kuanzia 130 na zaidi	Katika kila ngamia 40 atatoa bint labuun mmoja au katika kila ngamia 50 atatoa hiqqah mmoja.		

MASUALI KUHUSU ZAKAH

1. Haikubaliki zakah mpaka ipitiwe na mwaka wa takwimu ya.....
 - ☐ Hijri
 - ☐ Miladi
 - ☐ Hakuna tofauti baina ya takwimu zote mbili
2. Ni mali ipi sio lazima ipitiwe na mwaka?
 - ☐ Madini
 - ☐ Mazao ya ardhini
 - ☐ Vyote viwili
3. Kiwango cha dhahabu kinachofaa kutolewa zakah ni
 - ☐ Gramu 200
 - ☐ Gramu 595
 - ☐ Gramu 85
4. Kiwango cha fedha kinachofaa kutolewa zakah ni
 - ☐ Gramu 85
 - ☐ Gramu 959
 - ☐ Gramu 595
5. Mifugo wanaotolewa zakah ni 1.....2.....3.....4.....5.....
6. Je inapaswa kutoa zakah katika matunda?
7. Mifugo wanaotolewa zakah ni wale
 - ☐ Wanaoenda malishoni huru
 - ☐ Wanaoletewa lishe zizini pasina kutoka
8. Elezea tofauti ya fakiri na maskini.
9. Fakiri anapewa katika zakah lishe inayomtosha
 - ☐ Mwaka mzima
 - ☐ Mwezi mzima
10. Wakusanya zakah ni
11. Kafiri anayeogopwa kwa shari zake kwa Uislamu anapewa zakah?
12. Je kusamehe deni kwa nia ya zakah inakubaliwa?
13. Kujenga msikiti ni miongoni mwa sehemu zinazokubaliwa kutoa zakah?
14. Ni yupi katika wanyama hawa hatolewi zakah:-
 - ☐ Kuku
 - ☐ Paka
 - ☐ Farasi
 - ☐ Wote

15. Nyumba anayoishi mtu, kiwango cha kuitolea zakah ni ngapi?

- ☐ Thamani ya dhahabu
- ☐ Haitolewi zakah

16. Kila msafiri lazima apewe zakah?

- ☐ Ndio
- ☐ Hapana isipokuwa akiwa ni rafiki ya mkusanya zakah
- ☐ Hapana

17. Taja kiwango cha zakah kwenye mali ifuatayo:-

MALI	ZAKAH
Dhahabu gramu 100	
Dhahabu gramu 200	
Dhahabu gramu 400	
Dhahabu gramu 80	
Fedha gramu 500	
Mbuzi 30	
Mbuzi 60	
Mbuzi 565	
Ngamia 4	
Ngamia 17	
Ngamia 449	
Ng'ombe 30	
Ng'ombe 49	
Ng'ombe 77	
Ng'ombe 99	
Milioni 20 Ksh.	
Kilogramu 255 za ngano	
Kilogramu 600 za mchele	

TATU: SAUM (KUFUNGA)

Saum katika asili ya kilugha inamaanisha *kujizuia*

Katika Sheria inamaanisha *kujizuia chakula, kinywaji na mambo yote yanayofuturisha kwa nia ya ibada kuanzia kuingia AlFajr hadi kuzama jua.*

NGUZO ZA SAUM

NIA

KUJIZUIA NA VIFUTURISHI

NIA YA SAUM YA FARADHI

Lazima mtu anuwie usiku kabla ya alfajiri ya siku ya funga ile. Na inatosheleza kunuwia mwanzo wa mwezi wa Ramadhani unapoingia. Sehemu ya nia ni moyoni na wala haifai kuitamka maana itakuwa ni uzushi.

NIA YA SAUM YA SUNNAH

Inakubalika kunuwia wakati wowote ule wa mchana maadamu hajafanya chochote miongoni mwa vifuturishi.

AINA ZA SAUM

WAJIB

Ni aina tatu:-

1. Ramadhani
2. Kafara
3. Nadhiri

SUNNAH

Saum zote zisizokuwa za wajib.

MASHARTI YANAYOWAJIBISHA KUFUNGA

- | | | |
|--|----------------|--------------|
| 1 Uislamu | 2 Akili timamu | 3. Kubaleghe |
| 4 Ukaazi (asiwe msafiri) | 5 Afya | |
| 6 Kutokuwa katika hali ya kutokwa kwa damu ya hedhi au uzazi | | |

AINA ZA MARADHI KATIKA SAUM

MARADHI YASIOTARAJIWA KUPONA

Anaingia katika kitengo hiki mzee mkongwe ambaye hawezifunga: hawa hawalazimishwi kufunga ila wanalisha maskini mmoja kila siku ya Ramadhani. Kulisha kuna njia mbili:

1. Kuwakusanya jumla ya maskini kadri ya idadi ya siku za Ramadhani ile (29 au 30) na kuwalisha wote kwa pamoja.
2. Au awape maskini wote hao kila mmoja wao chakula (kwa mfano mchele) na iwe kipimo chake gramu 610. Na akizidisha chochote ni bora.

MARADHI YANAYOTARAJIWA KUPONA

Anaingia katika kitengo hiki mwanamke katika siku za hedhi, damu ya uzazi, anayenyonyesha na msafiri. Watahesabu jumla ya siku ambazo hawakuzifunga kisha atazifunga akipata wasaa wa kufunga. Na akifa kabla ya kulitelekeza hilo deni la funga, basi litakuwa limemwondokea dhima lake.

KUINGIA MWEZI WA RAMADHANI KUNADHIBITIKA KWA KITU GANI?

Inaingia ima kwa kuonekana mbalamwezi au kukamilika mwezi wa Shabani siku 30.

MAMBO YANAYOVUNJA SAUM

1. Kula na kunywa kusudi (*akila au kunywa kwa kughafilika basi saum yake ni sahihi*)
2. Kumuingilia mwanamke kwa tendo la ndoa; ikiwa ni mchana wa saum ya Ramadhani basi inamlazimu kafara ya kumwacha mtumwa huru au kufunga siku sitini mfululizo au kulisha maskini sitini.
3. Kutokwa manii kwa kumpapasa mwanamke au kumbusu au kujichua.
4. Sindano za lishe au vinywaji au mfano wake.
5. Kutoa damu kwa njia ya hijama. Lakini kutoa damu ndogo kwaajili ya vipimo haina shida.
6. Kujitapisha
7. Kutokwa kwa damu ya hedhi au uzazi.

BAADHI YA YANAYORUHUSIWA KATIKA SAUM

Kumeza mate, kuonja chakula kwa ulimi kwa dharura, kuoga, kuswaki, marashi na kujipa baridi

BAADHI YA YANAYOPENDEKEZWA KATIKA SAUM

- | | | |
|----------------------------------|---|----------------------|
| 1 Kula daku | 2 Kucheleweshwa daku | 3 Kuharakisha futari |
| 4 Kufuturu kwa tende za rutab au | tende za kawaida au maji na akikosa basi anuwie | |
| 5 Dua wakati wa kufuturu | 6 Kuzidisha sadaka | 7 Sala ya usiku |
| 8 Kuisoma Kur'ani | 9 Kutoingia katika ugomvi | 10 Umrah |
| 11 Itikafu msikitini | 12 Kuutafuta usiku wa Leilatul Oadri | |

BAADHI YA YANAYOCHUKIZWA KATIKA SAUM

1. Kupitiliza katika kusukutua na kuingiza maji puani
2. Kuonja chakula kwa ulimi pasina haja

BAADHI YA YANAYOHARAMISHWA KATIKA SAUM

- Kumeza kikohozi (lakini haifuturishi)
- Kumbusu mwanamke kwa asiyeweza kuizuia hamu ya nafsi yake.
- Uongo na maneno ya kipuuzi
- Kutofaidika kielimu katika mafunzo ya saum
- Kuzinganisha siku mbili au zaidi za saum pasina kufuturu

SAUM ZA SUNNAH

- Kuzifunga siku sita za mwezi wa Shawwal kwa aliyekamilisha funga ya Ramadhani. Inapendekezwa azifunge kwa kufatanisha zote sita.
- Kufunga siku ya Arafa kwa yule ambaye hayuko kwenye ibada ya Hijja.
- Kufunga siku ya Ashuraa pamoja na siku kabla yake au siku baada yake.
- Kufunga kila siku ya Jumatatu na Alhamisi ya kila wiki.
- Kufunga siku tatu za kila mwezi wa Kiislamu (Tarehe 13, 14 na 15)
- Kufunga siku na kuacha siku.
- Kufunga mwezi wa Muharram.
- Kufunga siku tisa za mwanzo wa mwezi wa Dhul Hijja
- Kufunga mwezi wa Shabani (lakini asiufunge wote)

SAUM ZINAZOCHUKIZA

Kuifunga siku ya Ijumaa pekee au Jumamosi pekee au Jumapili pekee; lakini saum ya Sunnah ikiwiana na moja ya siku hizi basi ataruhusiwa kufunga.

SAUM ZINAZOHARAMISHWA

- Kuikhusisha mwezi wa Rajab kwa saum.
- Kufunga siku mbili za Eid (Eid kubwa na Eid ndogo).
- Kufunga siku ya shaka: siku asiyokuwa na uhakika kama mwezi umeonekana au la
- Kuzifunga siku tatu baada ya Eid kubwa (Tarehe 11, 12 na 13 za Dhul Hijja).
- Kufunga mwaka mzima

SHERIA ZA KULIPA DENI KWA ALIYEPITWA NA BAADHI YA MASIKU

- Inapendekezwa azifunge kwa kufatanisha
- Aharakishe kuzilipa pindi tu anapopata wasaa na uwezo wa kufunga
- Haifai kulichelewesha deni hilo hadi Ramadhani ifuatayo bila ya dharura.
- Akichelewesha hadi Ramadhani ifuatayo bila udhuru basi atapata dhambi

ZAKATUL FITRI (ZAKAH YA KUFUNGUA)

Inapozama jua siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani, ni wajibu juu ya kila Muislamu; mkubwa kwa mdogo, kiume kwa kike, mtumwa na aliye huru. Lazima atoe zakah yake na ya kila anayemtegemea yeye. Na anapaswa mtu kutoa kibaba cha chakula kinacholiwa kwenye mji wake.

Lengo la kuwekwa zakah hli kwenye sharia ni:-

1. Kuziba mapungufu yaliyopatikana kwenye saum
2. Kuwasitiri na kuwakinaisha fukara na maskini ili wasiombe siku ya Eid.

MIDA YA KUTOA ZAKATUL FITRI

UNAORUHUSIWA

Kabla ya Eid kwa siku moja
au siku mbili

UNAOPENDEKEZWA

Baada ya sala ya AlFajr siku
ya Eid hadi kabla ya sala ya
Eid.

UNAOHARAMISHWA

Baada ya sala ya Eid

KIWANGO CHA ZAKATUL FITRI

Kibaba cha chakula kinacholiwa kwenye mji wake na haipaswi kutoa pesa au vitu vingine ambavyo sio vyakula.

KIBABA ni kilogramu mbili na gramu arbaini (2 kg 40 grams)

SALA YA EID

Ni faradhi kwa kila mmoja ila mwenye udhuru. Inasaliwa sala hii ya Eid baada ya kuchomoza jua kadri ya urefu wa mkuki na muda wake unaisha linapoanza kupinda jua. Na atakayepitwa na sala hii haina kulipa. Na katika Sunnah, sala hii inafaa isaliwe kwenye uwanja; nje ya majengo. Inaruhusiwa kuisali msikitini kwa dharura ya mvua na dharura zingine.

Inafaa mtu ale tende kwa idadi ya witri au ale chochote kile kabla ya kusali eid, ajitwahirishe na kujisafisha, ajifukize kwa manukato mazuri au marashi, avalie mavazi mazuri na aelekee kwenye mswala kwa njia moja na akirudi arudi kwa njia nyingine. Na haina shida kupongezana kwa kusema ***Taqabbala Allahu minnaa wa minkum*** (Allah aitakabali amali yetu).

Na inapendekezwa katika Sunnah mtu kuzidisha Takbir kuanzia usiku ule wa Ramadhani kukamilika na kila baada ya sala za faradhi pia azidishe hadi kusali Eid.

TAKBIR YA EID

Allahu akbar, Allahu akbar. Laa ilaaha illa Allah. Allahu akbar, Allahu akbar wa lillaahil hamd.

Sala ya Eid inasaliwa rakaa mbili kabla ya khutbah: katika rakaa ya kwanza, analeta takbiratul ihraam kisha analeta takbir sita baadake. Na katika rakaa ya pili, analeta takbir tano baada ya Takbir ya wakati wa kusimama kutoka sijda ya pili kabla ya kusoma Fatihah.

MASUALI KUHUSU SAUM

1. Nguzo za saum ni ngapi?
 - ☐ 2
 - ☐ 3
 - ☐ 4
2. Saum ni wajibu kwa mtu mwenye sifa nne hizi:-
 - 1.....
 - 2.....
 - 3.....
 - 4.....
3. Kila mgonjwa haruhusiwi kufunga?
4. Elezea hukumu ya mambo yafuatayo yanayohusiana na saum:-

JAMBO	HUKUMU YAKE
Kunuwia saum baada ya Alfajr	
Kufunga bila nia	
Saum ya mtoto	
Saum ya msafiri	
Saum ya mwanamke mwenye damu ya uzazi	
Saum ya mzee mkongwe	
Kula akiwa amefunga	
Sindano za lishe	
Dawa za maji za macho	
Sindano ya dawa	
Kutoa damu kwa njia ya hijama	
Kutapika	
Kumeza mate	
Kuonja chakula ili kujua kama kina chumvi	
Kulala mchana wa Ramadhani	
Kuoga mchana wa Ramadhani	
Kupumzika sehemu kwa nia ya ubaridi na upepo	
Kufukiza udi na ubani mchana wa Ramadhani	
Kupiga mswaki mchana wa Ramadhani	
Mtu anapaswa kula nini daku?	
Mtu anapaswa kufuturu kwa kitu gani?	
Sala ya Taraweh	
Umrah mwezi wa Ramadhani	
Kupitiliza katika kusukutua	
Kuunganisha saum siku mbili bila kufungua	

Kufunga siku sita za mwezi wa Shawwal	
Kufunga siku ya Arafa	
Kufunga siku ya shaka	
Kufunga siku ya Eid	
Kufunga siku tatu baada ya Eid kubwa (11, 12 na 13)	
Kufunga mwezi wa Muharram	
Kufungwa mwezi wa Rajab wote	
Kufunga mwaka	
Kufunga siku ya Ijumaa pekee	
Kuchelewesha deni ya saum hadi Ramadhani ifuatayo	

NNE: HIJJA

Hijja ni nguzo ya tano katika nguzo za Uislamu. Na ni ibada ya lazima kwa kila aliyetimiza masharti haya yote: Muislamu, akili timamu, aliye huru, mwenye uwezo. Na mwanamke anazidishiwa sharti lingine; awe na mahram wake akihitajia kusafiri kwa ibada ya Hijja..

Na **NGUZO ZA HIJJA** ni nne:-

IHRAAM

Hii ni nia anayoitia mtu wakati wa kuianza ibada ya hijja. Inakuwa sehemu maalum baadi ya kuvaliza mavazi ya ihram.

KUSIMAMA ARAFA

Kusimama katika uwanja wa Arafa siku ya tisa ya mwezi wa Dhul Hijja kuanzia kupinda kwa jua hadi kuchomoza kwa alfajiri siku ya Eid kubwa. Amesema Mtume, “*Hijja ni Arafa*”

TWAWAAF IFAADHWA

(Twawaaf ya ziara)
Inakuwa ruhusa kuifanya kuanzia baada ya kusimama Arafa.

SA^YI

Kukimbia baina ya milima ya Swafa na Marwa

AINA ZA KUTEKELEZA IBADA YA HIJJA

TAMATTU^

Hii ni kutia nia ya umrah kisha akatekeleza umrah kiukamilifu mwanzo katika miezi ya Hijja. Kisha anavalia tena mavazi ya ihraam na kutia nia ya Hijja ili kuingia kwenye ibada ya Hijja.
Na huyu inamlazimu kuchinja.

QIRAAN

Hii ni kutekeleza ibada ya umrah na Hijja kwa pamoja.
Huyu pia inampasa kuchinja.

IFRAAD

Hii ni kutekeleza ibada ya Hijja pekee.

MAMBO YANAYOWAJIBISHWA KATIKA KUTEKELEZA IBADA YA HIJJA

Atakayewacha moja katika mambo haya basi anailipa kwa kuchinja mbuzi na kuigawa baina ya maskini wa mji wa Makkah. Na haifai yeye kula katika nyama ile. Wajibu hizi ni:-

Kuhirimia na kuvaa mavazi ya Ihraam kwenye miiqaat (sehemu maalum)

Kusima kwenye uwanja wa Arafa hadi kuzama jua (kwa atakayesimama mchana)

Kulala kwenye uwanja wa Muzdalifa

Kulala kwenye uwanja wa Mina usiku kuanzia Eid hadi mwisho wa siku za kuchinja

Kurusha mawe (jamaraat)

Kunyoa nywele au kuzipunguza

Twawaf ya kuaga kwa anayetaka kuondoka Makkah hata lau ni baada ya mwezi. (isipokuwa mwanamke mwenye hedhi au damu ya uzazi)

NYAKATI NA SEHEMU ZA HIJJA NA UMRAH

NYAKATI

- Miezi ya Hijja ni:- Shawwal, Dhul Qa[^]adah na Dhul Hijja.
- Ibada ya Hijja ina mwezi wake maalum
- Ibada ya Umrah haina wakati maalum

SEHEMU

- **DHUL HULAIFAH:** ni kwa watu wa Madinah na watakaopitia Madinah.
- **JUHFA:** ni kwa watu wa kanda za Syria, Misri na watu wanaotoka magharibi.
- **QARNUL MANAAZIL:** kwa watu wa Najd
- **YALAMLAM:** kwa wanaotoka Yemen.
- **DHAATA IRQ:** kwa wanaotoka Iraq

MAMBO YANAYOPENDEKEZWA KATIKA KUTEKELEZA IBADA YA HIJJA

Kuoga na kujifukiza marashi kabla kuhirimia na kuvaa mavazi ya Ihraam kwenye miiqaat (sehemu maalum)

Kuvaa mashuka mawili (shuka na kikoi) meupe ya ihraam kwa wanaume.

Kukata kucha na baadhi ya nywele (kama kuna haja) kabla ya kuvaa mavazi na kabla ya kutia nia ya ihraam.

Kuleta talbiya kuanzia kunuwia ihraam hadi kuanza kurusha mawe (jamaraat)

Twawaaf ya Kufika (Kwa qaarin na ifraad)

Kutembea upesi katika twawaaf ya Kufika

Kupitisha ncha za shuka chini ya kwapa la kulia katika twawaaf ya Kuingia.

Kutanguliza katika kujumuisha baina ya sala ya Maghrib na sala ya Isha.

Kulala kwenye uwanja wa Mina usiku wa Arafa

Kuibusu Hajarul Aswad (jiwe nyeusi kwenye nguzo ya kulia ya Kaabah)

Kusimama kwenye uwanja wa Muzdalifa kwenye sehemu shiari tukufu kuanzia alfajiri hadi kupambazuka.

MAMBO YANAYOKATAZWA BAADA YA IHRAAM

Ni mambo tisa:-

Kunyoa nywele za kichwa na mwili, kukata kucha, kufunika kichwa kwa kitu kilichoshikana na kichwa kwa wanaume, nguo linalotenganisha viungo kwa wanaume, wanawake kuvaa nikabu na glavu, kujifukiza marashi au kutumia sabuni zenye manukato, kuwinda na kuwaua wanyama wa porini, kufunga ndoa au kufungisha ndoa, kufanya tendo la ndoa au kuhamasishana hisia bila kufanya tendo.

Atakayefanya haya kwa kusahau au kutojua au kulazimishwa basi hana dhambi isipokuwa atakayewinda au kumuua mnyama mwitu basi atalipa fidia sawa na alichokiua.

Ama atakayefanya mambo haya kwa kusudi basi kuna hali nne zitakazozingatiwa:-

KISICHOKUWA NA FIDIA

Kufunga au kufungisha ndoa. Na pia kuhamasisha hisia bila tendo la ndoa pasina kutokwa na manii. Haya yanahitaji tauba wala hayana fidia.

CHENYE FIDIA MFANO WAKE

Kuwinda au kumuua mnyama mwitu. Basi mtu huyu atalipa fidia mfano wa kile alichokiua au kukiwinda. Waadilifu wawili watakitathmini alichokiua.

CHENYE FIDIA NZITO

Kufanya tendo la ndoa. Atakayemuungilia mke wake kabla ya uhalalisho wa ibada wa mwanzo basi huyo imeharibika Hijja yake na inamlazimu kuikamilisha na atairudia mwaka mwingine. Na inamlazimu kichinjo.

CHENYE FIDIA YA UDHIO

Mambo mengine yaliyobakia. Fidia yake atachagua baina ya kufanya moja katika matatu haya:-

- Kufunga siku tatu
- Kulisha maskini sita kila mmoja wao pishe ($\frac{1}{2}$ kg)
- Kuchinja mbuzi na kuigawa kwa maskini wa Makkah.

MAJINA YA SIKU ZA HIJJA

1. **TARWIYAH:** hii ni siku ya nane ya mwezi wa Dhul Hijja. Walikuwa masahaba wakibeba maji kupeleka uwanja wa Mina.
2. **ARAFa:** hii ni siku ya kisimamo. Na inakuwa siku ya tisa ya mwezi wa Dhul Hijja.
3. **EID NA NAHR:** hii ni siku ya Eid kubwa. Ni siku ya kumi ya mwezi wa Dhul Hijja
4. **QARR:** siku ya kumi na moja ya mwezi wa Dhul Hijja (siku ya kwanza ya Tashriiq)
5. **FARRI YA KWANZA:** siku ya kumi na mbili ya mwezi wa Dhul Hijja. Siku hii wanarahusiwa kikundi cha kwanza wenye haraka kuondoka.
6. **FARRI YA PILI:** siku ya kumi na tatu ya mwezi wa Dhul Hijja. Siku hii waliobaki wanarahusiwa kuondoka; ni siku ya mwisho katika ibada za Hijja.

SEHEMU MUHIMU ZA KUOMBEA DUA KATIKA IBADA YA HIJJA

ARAFa

Katika uwanja wa Arafah, siku ya Arafah, baada ya jua kupinda hadi magharibi.

MUZDALIFA

Siku ya Arafah baada ya alfajiri hadi kupambazuka.

RAMYU

Baada ya kurusha mawe (ndogo na za kati)

TWAWAAF

SA^YI

Katika mbio za Swafa na Marwa na sehemu baina yao.

SIFA YA HIJJA NA UMRAH

Amesema Sheikh Muhammed bin Swalih Uthaimin, Allah amrehemu:

Akifika mtu kwenye miiqaat basi aoge na ajifukize manukato na marashi mwilini na kichwani. Kisha ahirimie (avalie mavazi ya ihraam na anuwie anachokikusudia katika Hijja au umrah). Kisha aende Makkah kwa talbiyah. Akifika msikiti mtukufu wa Makkah aanze twawaaf kwa kuizunguka Kaabah mara saba. Na afahmu kuwa msikiti wote ni sehemu anaweza kufanyia twawaaf, lakini akiweza kufanyia karibu na Kaabah ni bora zaidi kama haitoleta maudhi au msongamano. Akimaliza twawaaf, atasali rakaa mbili nyuma ya masimamo ya nabii Ibrahim (*maqaam Ibrahiim*) kwa ukaribu au mbali; la muhimu ni kuwa masimamo yawe baina yake na Kaabah. Kisha baada ya hapo, ataenda kwenye Sa^yi aanze na mlima wa Swafa akielekea Marwa; mara saba. (Swafa hadi Marwa ni mara moja na kutoka Marwa kuja Swafa ni nyingine). Akishamaliza apunguze

nywele zake za kichwani kwa usawa na haifai kupunguza baadhi ya pande na kuziacha zingine. Ikifika siku ya nane ya Dhul Hijja, aoge, ajifukize na ahirimie kwaajili ya Hijja sehemu alipo. Kisha aelekee Mina asali huko sala ya Dhuhur, Asr, Maghrib, Isha na Fajr (kwa kupunguza sala za rakaa nne ziwe mbili).

Ikichomoza jua siku ya Arafa, wataondoka kwa unyenyekevu kuelekea uwanja wa Arafa huku wakizidisha utajo na talbiyah. Watajumuisha sala ya Dhuhur na Asr kwa muda wa Dhuhur pamoja na kuzifupisha. Kisha watatokomea kwenye kumuomba Allah na kujikurubisha Kwake na ajitahidi mtu awe kwenye hali ya twahara na aelekee Qiblah kama ilivyo kwenye sheria. Na awe makini sana aizingatie mipaka ya uwanja wa Arafa na alama zake kwa sababu wingi wa mahujaji wanadhani wamesimama uwanjani Arafa kumbe wako nje ya uwanja na wakaikosa Hijja. Kwa sababu anasema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, “*Hijja ni arafa*”. Na uwanjani Arafa kote kunaruhusiwa kusimama isipokuwa ndani ya bonde.

Jua likizama kiuhakika, aondoke kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na unyenyekevu kama ilivyoamrisha. Wakifika huko Muzdalifa, watasali Maghrib na Isha kisha watapumzika hadi Alfajr na haruhusiwi mtu yeyote kutoka kabla ya Alfajr isipokuwa wenye udhaifu au majukumu ya huduma.

Akishasali Fajr, ataelekea Qiblah kwa utajo na dua hadi kupambazuke vyema kisha ataondoka kuenda Mina. Atakusanya mawe madogo saba aelekee Jamara Kubwa, iliyoko mwisho karibu na Makkah, arushe mawe yale kwa Takbir kila akirusha kimoja. Ahakikishe mawe yote yametumbukia kwenye ukanda ule wa nguzo la Jamara.

Akimaliza, atachinja kwa kuzingatia masharti ya uchinjaji na inaruhusiwa amwakilishe mtu kumtekelezea shughuli ile ya uchinjaji. Kisha atanyoa nywele zote za kichwani kwa usawa baada ya kuchinja na haifai kunyoa baadhi ya sehemu tu. Na mwanamke ananyoa nywele kidogo tu kadri ya kichwa cha kidole cha gumba. Na akitimiza hayo basi atakuwa amefikia **uhalalisho wa mwanzo**. Basi hapo anaweza akavaa mavazi ya kawaida, kukata kucha, kujifukiza marashi isipokuwa tu haruhusiwi kufanya tendo la ndoa. Kisha ataelekea msikitini kabla ya sala ya Dhuhur afanye twawaaf na sa[^]yi, kisha atarudi Mina. Kwa kutimiza twawaaf hiyo na sa[^]yi atakuwa ameingia **uhalalisho wa pili** ambapo sasa amehurusiwa kila kitu hata kufanya tendo la ndoa na mkewe.

Enyi watu! Hakika ya mambo anayoyafanya mtu siku ya Eid katika ibada ya Hijja ni mambo manne kuu: kuchinja kisha kunyoa kisha twawaaf na sa[^]yi. Na huu ndio utaratibu bora lakini akitanguliza yeyote katika mambo hayo mbele ya nyingine haina tatizo. Na lau akichelewesha kuchinja hadi siku ya kumi na tatu ya Dhul Hijja hakuna tatizo pia.

Kisha kwa siku atakazokuwa Mina atarusha mawe ishirini na moja kila siku kwa kila jamara mawe saba. Na anaruhusiwa kuondoka baada ya kurusha mawe siku ya 12.

Na akitaka kuondoka Makkah, aende afanye twawaaf ya kuaga isipokuwa tu kwa mwanamke mwenye hedhi na damu ya uzazi.

MASUALI KUHUSU HIJJA

1. Hija ni lazima kwa mwenye sifa hizi:
 - 1.....
 - 2.....
 - 3.....
 - 4.....
2. Mwanamke ana ziada ya sharti moja ambalo ni
3. Nguzo za Hija ni ngapi?
 - ☐ 2
 - ☐ 3
 - ☐ 4
4. Ihraam katika nguzo za Hija inamaanisha
5. Twawaaf ni nini?
6. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alifanya Hija ngapi?
7. Watu wa Madinah wanahirimia Yalamlam. (sahihi / sio sahihi)
8. Mwezi maalum wa Umrah ni Ramadhani.(sahihi / sio sahihi)
9. Ni wajibu mtu kutekeleza Hija mara ngapi katika umri wake?
 - ☐ Kila mwaka
 - ☐ Mara tatu
 - ☐ Mara moja
 - ☐ Kila mwezi
10. Watu wa Makkah wanahirimia wapi?
11. Mwanamke anavalia mavazi ya ihraam meupe. (sahihi / sio sahihi)
12. Je. inafaa mwanamke kuvaa nguo lililoshonwa lenye kutenganisha viungo?
13. Haifai kufunga mkanda/mshipi kwa mwanamume.(sahihi / sio sahihi)
14. Hija inaanza siku ya na kuisha siku ya
15. Kusimama katika uwanja wa Arafah ni
 - ☐ Nguzo
 - ☐ Sharti
 - ☐ Wajib
16. Je ni lazima mtu kuupanda mlima wa Arafah?
17. Ni lazima qarin kuchinja. (sahihi / sio sahihi)
18. Je Hija ya mtoto inakubaliwa?
19. Je Hija ya mwanamke bila mahram wake inakubalika?
20. Kukopa deni ili kuenda Hija inakubalika?

SOMO LA KUMI NA TANO

KUSIFIKA KWA TABIA NJEMA

Kila Muislamu ni wajibu asifike kwa tabia njema za kidini. Miongoni mwa tabia njema ni: kuwa mkweli, kutunza amana, kuzuia matamania, kuwa na haya, ushujaa, ukarimu, utekelezaji ahadi, kujiepusha na alichoharamisha Allah, ujirani mwema, kusaidia wenye haja kadri ya uwezo na mengineo katika tabia njema zilizofunzwa kwenye Kur'ani na Sunnah.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA TABIA HIZI

- **UKWELI:** awe mkweli na Allah katika maneno yake, vitendo vyake na itikadi yake. Pia awe mkweli na waja katika kuamiliiana nao. Kinyume chake ni uongo.
- **AMANA:** hii ni faradhi kubwa na jukumu kubwa alilojitwika mwanadamu. Kinyume chake ni khiana.
- **KUJIZUIA MATAMANIO:** kujizuia kuangukia katika makatazo.
- **HAYA:** ni jambo linalompelekea mtu kufanya nzuri na kuachana na mabaya.
- **UJIRANI MWEMA:** na katika ujirani mwema ni kuhifadhi macho na kutoangalia na kutochunguza siri na madhaifu ya jirani.
- **KUSAIDIA WENYE HAJA:** amesema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, *“atakaye muondoshea ndugu yake uzito miongoni mwa uzito wa duniani basi Allah atamuondolea uzito wa siku ya Kiyama.....na atakayesitiri aibu ya Muislamu basi Allah atasitiri aibu yake siku ya Kiyama”* (Ameipokea Muslim)

SOMO LA KUMI NA SITA

KUISHI KWA ADABU ZA KIISLAMU

Miongoni mwa adabu za Kiislamu ni: kutoa salamu, bashasha, kula kwa mkono wa kulia, kunywa kwa mkono wa kulia, kutaja jina la Allah mwanzo wa kila jambo, kumshukuru Allah baada ya kumaliza jambo, kumhimidi Allah baada ya kupiga chafya, kumuomba mpiga chafya akishukuru, kumzuru mgonjwa, kufuata jeneza kwaajili ya sala na mazishi, adabu za kisheria wakati wa kuingia nyumbani na kutoka, wakati wa safari, ukiwa na wazazi na familia na ukoo, majirani, waliokuzidi umri na wadogo zako, kumpongeza aliyeruzukiwa mtoto, kumtakia baraka aliyefunga ndoa, kumliwaza aliyefiwa na adabu zingine katika mavazi.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA ADABU HIZI

- **SALAMU:** kumtolea salamu anayemjua na asiyemjua na kujibu salamu akisalimiwa.
- **KULA NA KUNYWA KWA KULIA:** ni wajibu kula na kunywa kutumia mkono wa kulia na vilevile kukabidhi au kupokea kitu. Na ale kilicho karibu naye wala asiwe na tamaa wala pupa.
- **JINA LA ALLAH KWA KILA JAMBO:** alitaje jina la Allah kabla ya kuanza jambo lolote ili liwe na baraka na kheri ndani yake.
- **KUMSHUKURU ALLAH BAADAKE:** arudishe shukrani kwa Allah akishamaliza jambo lile ili Allah apate kumzidishia.
- **AKIPIGA CHAFYA:** aseme *Alhamdu Lillah*
- **KUMUOMBEA MPIGA CHAFYA:** mpiga chafya akisema *Alhamdu Lillah* basi yeye amwambie *Yarhamuka Allah* (Allah akurehemu)
- **KUMZURU MGONJWA:** azidishe ziara yake kwa mgonjwa kwa nyakati zinazofaa. Wala asiketi sana akamuudhi na wala asimkatishe tamaa na rehema za Allah.
- **KUFUATA JENEZA:** inaruhusiwa kwa wanaume na sio ruhusa kwa mwanamke.
- **KUINGIA NA KUTOKA MSIKITINI:** autangulize mguu wake wa kulia na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillah. Allahumma iftah lii abwaaba rahamtika* (Kwa jina la Allah. Rehema na amani zimwendee mjaWake na Mtume Wake. Mola wangu nifungulie milango ya rehema Yako.)
Na akitoka autangulize kushoto na aseme: *Bismillahi wa sswalaatu wa ssalaam alaa rasuulillah. Allahumma inniy as-aluka min fadhlika.* (Kwa jina la Allah. Rehema na amani zimwendee mjaWake na Mtume Wake. Mola wangu nakuomba unipe katika fadhila Zako)
- **KUTOKA NYUMBANI:** atangulize mguu wa kulia wakati wa kuingia na wakati wa kutoka na asome nyiradi za kuingia na zile za kutoka nyumbani.

SOMO LA KUMI NA SABA

KUJITAHADHARISHA NA SHIRKI NA AINA ZA MAASI

Kuhadhari na kujitahadhirisha kutokana na shirki na aina za maasi:

Miongoni mwake **MADHAMBİ SABA KUBWA** ambayo ni: shirki, uchawi, kuua nafsi bila haki, kula riba, kula mali ya yatima, kutoroka uwanja wa jihad na kuwasingizia zinaa wanawake waumini waliojihifadhi.

Na miongoni mwa madhambi pia ni: kuwaasi wazazi wawili, kukata undugu, ushahidi wa uongo, kiapo cha uongo, kumuudhi jirani, kuwadhulumu watu katika damu, mali na heshima zao, ulevi, kucheza kamari, kusenganya, kufitinisha watu na mengine aliyoyakataza Allah na Mtume Wake.

UFAFANUZI MFUPI WA BAADHI YA YALIYOTAJWA

- **SHIRKI:** inakusanya shirki kubwa na shirki ndogo.
- **UCHAWI:** atakayefanya uchawi au akaridhia uchawi basi amekufuru. Na inaharamishwa kuwaendea wachawi au kuwazuru ili kushuhudia mambo yao au kutizama vipindi vyao, kusoma jarida lao au kujihusisha kwenye miradi yao. Na haifai kutengua uchawi kwa kutumia uchawi bali uchawi hutenguliwa kwa ruqya ya kisheria na mafunzo yaliyopokelewa.
- **UUWAJI WA NAFSI BILA HAKI:** haifai kuuwa nafsi ya Muislamu wala kafiri. Inaruhusiwa kuuwa nafsi kwa sababu tatu: akiua nafsi, akiritadi au akizini hali ya kuwa ameo/ameolewa.
- **KULA MALI YA YATIMA:** yatima ni yule aliyempoteza (kufa) babake yake kabla ya kubaleghe.
- **KUTOROKA UWANJA WA JIHAD:** jeshi walioko vitani.
- **KUWASINGIZIA ZINAA WAUMINI:** waliojihifadhi.
- **KIAPU CHA UONGO:** vilevile kuapa kwa asiyekuwa Allah au kaburi.
- **KAMARI:** kila aina ya kamari ambayo ina chumo lililokatazwa kisheria.
- **KUSENGENYA:** ni kumtaja ndugu yako kwa lile asilolipenda
- **KUFITINISHA WATU:** kuhamisha maneno baina ya watu kwa nia ya kusababisha ugomvi baina yao.

HUKUMU YA MASHINDANO

YALIYOHARAMISHWA

Kamari kwa aina zake zote za kitambo na za kisasa.

**INARUHUSIWA KWA
MBADALA NA BILA
MBADALA**

Kama mashindano ya mbio za farasi na ngamia

**INARUHUSIWA BILA
MBADALA NA
HAIRUHUSIWI KWA
MBADALA**

Michezo yote kando na zilizotajwa

SOMO LA KUMI NA NANE

MAANDALIZI YA MAITI, SALA YAKE NA MAZISHI

Maandalizi ya maiti ni kwa mambo yafuatayo:-

KWANZA : inafaa kumkaririsha maiti (talqiin) ya shahada kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, “*wakaririsheni maiti wenu laa ilaaha illa Allah*” maana ya maiti katika hii ni yule mtu yupo kwenye kitanda cha mauti/ yamemfika wakati wa kuaga dunia.

PILI : ikisha kuwa uhakika kuwa amekufa, basi afungwe macho yake.

TATU : ni jambo la lazima kuoshwa maiti wa Kiislamu isipokuwa tu yule aliyekufa katika uwanja wa jihad; huyu haoshwi wala hasaliwi na atazikwa katika mavazi yake aliokufa nayo. Dalili ya hili ni kuwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, hakuwaosha waliokufa kwenye vita vya Uhud wala hakuwasalia.

NNE : SIFA YA KUMUOSHA MAITI: asitiriwe uchi wake, kisha anyanyuliwe kidogo ili kulikamua tumbo lake kwa utaratibu. Kisha muoshaji ataweka funda la maji mkononi ili amchambishe maiti. Kisha atatawadhishwa kama Wudhuu wa sala. Kisha atakoshwa kichwa chake na ndevu zake kwa maji na kafuuri au chochote kile katika vitu vyenye harufu nzuri. Kisha ataoshwa ubavu wake wa kulia kisha wa kushoto. Kisha ataoshwa hivyo pande zote mbili kwa mara tatu; katika kila muosho, ataupitiza mkono wake tumboni taratibu ili kuhakikisha hakuna uchafu utokao tumboni. Uchafu ukitoka atausafisha na ukizidi kutoka basi atamziba tundu zile kwa pamba au udongo au njia ya kisasa kisha atamtawadhisha tena. Na isipotosheleza kumuosha mara tatu basi muoshaji atazidisha kadri ya haja. Kisha atamkausha maji mwilini kutumia ngua au kitambaa kisha atamnyunyizia marashi mwilini hasa chini ya kwapa, baina ya mapaja na kwenye viungo vya sijda. Kisha sanda zake zitafukizwa kwa udi au ubani. Ikiwa masharubu yake au kucha zake ni ndefu basi zitakatwa. Na zikiachwa pia hamna tatizo. Wala asinyolewe nywele za kichwani wala za sehemu za siri wala asitahiriwe.

TANO : KUMKAFINI MAITI: iliyo bora ni kumkafini maiti wa kiume kwa sanda tatu (billa kanzu wala kilemba) kama alivyokafiniwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake; kila sanda inaingizwa ndani ya nyingine. Na ikiwa ni maiti ya kike basi atakafiniwa kwa sanda tano: dera, shungi, mtandio na shuka mbili.

Inatosheleza kumkafini mtoto kwa sanda moja hadi tatu.

Na pia inatosheleza (wajib) maiti yeyote kuvishwa sanda moja ikitosha kuusitiri mwili mzima.

Ikiwa maiti mwanamume alikufa katika ibada ya hijja basi ataoshwa kwa maji na kafuuri na atakafiniwa kwa mavazi yake ya ihraam au mavazi mengine bila kufunikwa kichwa wala uso wala kufukizwa marashi kwa sababu atafufuliwa siku ya Kiyama hali ya kuwa anatoa utajo.

Lakini ikiwa ni maiti mwanamke aliyekufa katika ibada ya Hijja, basi huyu atakafiniwa kama maiti wengine wa Kiislamu bila kufukiziwa marashi wala kufunikwa usoni kwa nikabu wala kuvishwa glavu lakini atafungwa kwa mavazi aliyokuwa amevaa kama ilivyotangulia.

SITA : wenye haki zaidi katika kumuosha maiti ni: aliohusiwa na maiti kisha babake kisha babu yake kisha wa karibu katika wanaume hadi mwisho ikiwa maiti ni mwanamume. Ikiwa maiti ni mwanamke, basi wenye haki zaidi katika kumuosha ni: aliohusiwa na maiti kisha mamake kisha bibi yake kisha wa karibu hadi mwisho katika wanawake.

Ni ruhusa baina ya wana ndoa wawili kuoshana akifa mmoja wao kama vile Abubakar, Allah awe radhi naye, alivyooshwa na mkewe na kama vile Ali, alivyomuosha mkewe Fatuma, Allah awe radhi nao.

SABA : sifa ya sala ya jeneza: inakuwa na Takbir nne: Baada ya Takbir ya kwanza atasoma suratul Fatihah; na akisoma baadake surah nyingine fupi pia haina tatizo. Kisha baada ya Takbir ya pili atamsalia Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. kisha baada ya Takbir ya tatu atamuomba maiti dua akisema: *Allahumma ighfir lihayyinaa wa mayyitinaa, wa shaahidinaa wa ghaaibinaa, wa swaghiirinaa wa kabiirinaa, wa dhakarinaawa unthaanaa. Allahumma man ahyaitahu minhu fa-ahyihi alal Islaam. Wa man tawaffaitahu minnaa fatawaffahu alal iimaan. Allahumma ighfir lahu wa-r-hamhu wa aafihi waifu anhu wa akrim nuzulahu, wa wassi' mudkhalahu, wa-ghsilhu bilmaai wa thalji wal barad. Wa naqqihi minal khatwaayaa kamaa yunaqqaa th-thaubul abyadh mina ddanas. Wa abdillhu daaran khairan min daarihi, wa ahlan khairan min ahlihi, wa adkhillul jannah wa a-idh-hu min adhaabil qabri wa adhaabi nnaar. Wa-f-sah lahu fii qabrihi wa nawwir lahu fiihi. Allahuma laa tahrinnaa ajrahu wa laa tudhwillunaa ba'dahu.* Kisha ataleta Takbir ya nne atatoa salamu moja upande wakulia. Katika Sunnah ni imam asimame upande wa kichwa cha maiti ikiwa maiti ni wa kiume na katikati ya mwili wa maiti akiwa wa kike.

- NANE** : Sifa ya kuzika: katika sharia inafaa kuchimba kaburi fiti sita na ndani kuchimbwe mwanandani (*lahd*) ikielekea Qiblah. Maiti alazwe kwenye mwanandani kwa ubavu wake wa kulia pamoja na kulegeza kanda zilizoshikilia sanda bila ya kutolewa. Wala haipaswi maiti kufunuliwa uso awe mwanamke awe mwanamume. Kisha ataegezewa udogo wa matope au tofali la kushikilia mwili usipinde au chochote kile au mbao kisha kumwaga mchanga. Inapendekezwa kusema wakati wa kumuingiza maiti kaburini: *Bismillahi wa alaa millati rasuulillah*. Kaburi lifukiwe na linyanyuliwe kadri shibiri moja na liwekwe alama kuonyesha kaburi na kunyunyiziwa maji ikiwezekana.
- TISA** : inaruhusiwa kwa yule ambaye hakuwahi sala ya jeneza, atamsalia baada ya kuzikwa kama alivyofanya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. (lakini iwe ndani ya mwezi mmoja baada ya mazishi)
- KUMI** : haifai familia ya maiti kuandaa chakula cha hitma isipokuwa kwa sababu ni kinyume na mafunzo ya dini. Bali ni wajibu wa ndugu zao na majirani kuwaandalia familia.
- KUMI NA MOJA** : haifai mwanamke kukaa hidda ya kuomboleza karibu wake zaidi ya siku tatu isipokuwa tu mumewe ambaye ataketi miezi mine na siku kumi. Isipokuwa kama mumewe alikufa akiwa mjamzito baasi hidda ya (kukaa ndani bila ya kujipamba) hadi ajifungue.
Ama mwanamume, hana kuketi hidda kabisa.
- KUMI NA MBILI** : inaruhusiwa wanaume kuzuru makaburi kwa lengo la kuwaombea wafu, kuwatakia rehema na kujikumbusha na akhera kama alivyosema Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, “*Zuruni makaburi, hakika kuzuru huko kutawakumbusha akhera.*” Na alikuwa akiwafunza masahaba zake wakizuru makaburi waseme: *Assalamu aleikum ahla diyaar minal mu’miniina wal muslimiin. Wa innaa in shaa Allah bikum laahiquun. Nas-alu Allaha lanaa wa lakumul aafiyah. Yarhamu Allahu almustaqdimiina wal musta’khiriin.*
Wala hawaruhusiwi wanawake kuzuru makaburi kwa kaui ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, “*Wamelaaniwa wanawake wenye kuzuru makaburi.*” Na kwa sababu pia wanawake ni wepesi wa kufitiniwa na wepesi wa subira. Na vivyo hivyo hawapaswi kufuata jeneza hadi makaburini kwa katazo la Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.
Na ni ruhusa kusaliwa maiti msikitini au kwenye muswala kwa wa kike na kiume.
Kwa haya machache, Allah atuwafikishe katika kila kheri na atusamehe kwa kila kosa.

AINA ZA ZIARA MAKABURINI

ZIARA YA KISHIRKI	ZIARA YA KIZUSHI	ZIARA YA KISHERIA
Ziara kwa nia ya kumuomba au kumuabudu au kujikurubisha kwa maiti kwa kutaka msaada wake.	Ziara kwa nia ya kumuomba Allah kwenye makaburi.	Ziara kwa nia ya kujikumbusha akhera. Wala haifai kufunga safari kwa sababu kuenda kuzuru makaburi. Na anapozuru makaburi basi awaombee wafu na awatakie rehema na asifanye jambo linaloenda kinyume na sharia.

MASUALI KWA YALIYOTANGULIA

1. Kuhifadhi nidhamu na adabu za kidini ni katika tabia za Muislamu..... (sahihi / sio sahihi)
2. Dini yangu inaniamrisha kufanya urafiki na waovu. (sahihi / sio sahihi)
3. Uislamu unatufunza kuwa wema katika kuamiliiana na watu. (sahihi / sio sahihi)
4. Je. Inaruhusiwa kufanya urafiki na mtu mwenye kuwaudhi watu?
5. Akinishtumu mtu inafaa nimshtumu pia. (sahihi / sio sahihi)
6. Uislamu unatufunza kuwasaidia wenye haja na wenye madhaifa..... (sahihi / sio sahihi)
7. Katika haki za Muislamu juu ya Muislamu mwenzake ni kumzuru akiwa mgonjwa?
8. Kuchunguza siri za majirani ni katika mafunzo ya dini yetu..... (sahihi / sio sahihi)
9. Ni mtu yupi anayependwa na Allah zaidi?
10. Dua ya kutoka nyumbani ni ipi?
11. Dua kwa mpiga chafya ni gani?
12. Nyiradi anazozihifadhi Muislamu zinamkurubisha kwa Allaha. (sahihi / sio sahihi)
13. Dalili za kuonyesha unampenda ndugu yako Muislamu ni?
14. Katika upungufu wa imani: kumhusudu ndugu yako Muislamu?
.....
15. Aina za mapenzi ni
16. Je. Ni haramu mtu kutumia kilevi?
17. Inachukiza kupumulia chakula au kinywaji..... (sahihi / sio sahihi)
18. Inaruhusiwa kuramba vidole baada ya kula..... (sahihi / sio sahihi)
19. Sifa ya mavazi ya Kiislamu ni
20. Ni nani mwenye haki sana kumuosha maiti?
21. Kulipa deni za maiti ni
☐ Lazima
☐ Inapendekezwa
☐ Inaruhusiwa
22. Hukumu ya kumzika maiti ni
☐ Inapendekezwa
☐ Lazima
☐ Faradhi ya kutosheleza ikifanywa na baadhi ya watu
23. Hukumu ya kumlakinisha maiti shahada ni
☐ Lazima
☐ Sunnah
☐ Haramu
24. Kumuosha maiti ni
25. Maiti anafaa kuvuliwa sanda akiwekwa kaburini?
26. Haifai wanandoa wawili kumuosha mwenziwe akifa..... (sahihi / sio sahihi)
27. Atakayepitwa na sala ya jenenza
28. Kupiga mayowe msibani ni
29. Maiti anaelekezwa Qiblah ndani ya mwanandani..... (sahihi / sio sahihi)